Commission ino ielewe kuwa kama Waislamu waumini dini yetu haitupi hiari ya kufuata jambo lolote likiwa limetoka kwa Mwenyezi Mungu na MTume wake. Kwa maana nyingine ningependa kuiomba Commission ino isisitize kama kipande cha Katiba na sheria kuwa kutungwe Katiba yoyote, kutungwe sharia zozote nchini Kenya zikihusiana na wengine lakini iwapo Katiba ino na sheria hizi zitapingana na Korahani tukufu na mwenendo na mafunzo ya MTume Mohammed, sisi Waislamu hatutakuwa na budi ila tuwe tutafuata Korahani na mafunzo ya MTume Mohammed . kwa lugha nyingizne ikiwa sheria au Katiba ya Kenya itapingana na sheria na Katiba ya Kiislamu sisi tutafuata ya dini, tutaweza kupuuza ya Kenya kwani tunaamini ni haki yetu. Hii ni upande mmooja.

Sasa tunakuja kwenye haki za wenyeji wa sehemu ino, ningependa zaidi kuwafafa nulia jambo ma Commissioner kwani kumetajwa mkataba baina ya Kenyatta na Shamte, mkataba uno ni wa tarehe tano October mwaka elfu moja mia tisa na sitini na tatu na nitawapa kopi wa mkataba wenyewe niko nao hapa. Nitawapa paia karatasi kuhusu mwakilishi wa Sultan ambao ako under the colonial office letter head alivyosema kuhusu wenyeji wa sehemu ino, nitawapa minutes za mkutano wa tatu wa Lancaster ambao ulikuwa umejadili na Kenyatta akakubali kuwa atalinda na atahifhadi haki za wenyeji halisi wa sehemu ino na nitawapa na memorandum ya waakilishi wa sehemu ino kwenye mkutano huo. Jambo la muhimu sana nikianza na uhuru wa kuabudu ambao ni sehemu ya kwanza ya mkataba huo. Umesisitiza kuwa institutions, tahasisi za Waislamu kwanza kutakuwa na uhuru wa dini na kwa Waislamu watakuwa na haki ya kusimamia ufundi na kuendesha tahasisi zao. Hili jambo kutoka Kenya ipate uhuru ni masitikiko yangu na ninahakika ya Waislamu wengi kuwa wame puuza na la kusikitisha zaidi yule aliye sign, Kenyatta alipuuza lakini na Raisi Moi alikuweco mkutanoni na yeye kutoka achukue chama cha uongozi hajajaribu kuhakikisha maneno haya yamezungumzwa na kutekelezwa.

Tatu, wajumbe wetu kwenye Bunge hawajasema lolote kuhusu mikataba ino aidha kwa kuwa hawajui au waogopa. Kwenye kifungu cha kwanza ni uhuru wa ibada, kifungu cha tano ni kuhusu haki za kumiliki ardhi yasiopaswa kulipa kodi. Free hold titles baada ya Kenya kupata uhuru wenye free hold titles walipuuzwa na wakatozwa kodi na serikali na hii ni kinyume cha mkataba uno baina ya Kenya na wenyeji halisi wa sehemu ino. Kwa maana ino tungependelea zaidi mkataba uno nyinyi ma Commissioners muutie maanani na muhakikishe:-

- (a) Kenya imetueleza kwa nini imepuuza.
- (b) Baada ya kuupuza afari ambayo imetupita wenyeji wa sehemu ino, Kenya itairekebisha na kutulipa vipi?
- (c) Waakikishe mkataba uno umetekelezwa kama ipasavyio.

Tunakuja kwenye Wakfu commssion. Kama alivyoeleza ndugu yangu Sheikh Halifah ino ni hazina ya Waislamu lakini kutokana na Wakfu Commissioners Act Chapter 109 inatoa rufusa ya kubuniwa, to establish an independent body ambayo ina watu wannane. Katika watu wanane hawa wote ni appointees wa serikali na wakichaguliwa wanaenda kwa PC yeyote wa Pwani, PC atawapeleka kwa Attorney General, Attorney General atawaidhinisha. Mjadala huu tunaupinga kwa sababu PC wa Pwani na Attorney General kisheria ya dini yetu hawaruhusiwi kusimamia pesa zetu.

Tunakuja kwenye appointment ya Chief Kadhi, natumaye ma Commissioner nyote mnajua kwamba Chief Kadhi nchini Kenya anachaguliwa na Judicial Service Commission. Kwa maana ino nitakuwa nafikiri si kukosea nikisema chief Kadhi ni:- (a) mfanyi kazi wa serikali (b) anawakilisha serikali kwenye jamii ya Waislamu kuhusu maswala ya dini ya Islamu na Waislamu wenyewe. Kinyume na sheria za dini ya Islamu, Chief Kadhi anatakikana awe ni msimamizi wa sheria na mamlaka ya dini ya Islamu awakilishe Waislamu kwenye serikali. Kwa maana ino ningepomba pia Tume ino isisitize kwenye Katiba kuwa Chief Kadhi iwe hatachaguliwa na serikali na yuapo atachaguliwa na serikali sisi tutakuwa hatumutambui.

Kuhusu ndugu yangu hapa ambaye amewakilisha disabled, ningependa kuisitiza Tume kama itilie maanani sana kuwasaidia walemavu wa aina tofauti, wawe ni wanawake au ni wananume, waweze kuwabunia na kuendeleza infrastructure yao kwa mfano mabasi ambao watakuwa wanapanda wao peke yao na vituo vingine vya huduma tofauti ambavyo vitakuwa ni vya wasio jiweza. Hili ndio ningependa kuisitiza kwa niaba ya walemavu.

Tukija kwenye issue ya Waswahili ambao Ni wenyeji halisi wa sehemu ino ya mwamba wa pwani, mimi mwenyewe wakati nilipokuwa nataka kuchukua kitambulisho nilipingana sana na ma clerk au makarani waliokuwa wakiandikisha kwa kutaka kunilazimisha niitwe Swahili Shirazi. Waswahili waheshimiwa hapa wako makabila kumi na mbili, makabila haya yako kwa tabaka kwa mfano kuna Wagunya, Wafaza, Wafafi, Wakatwa, Washaka, Wakilifi, Wamtwapa, Wamvita, Wakilindini, Wachangamwe, Watangana, na Wanjoni. Bali ya kuwa katika kabila Waswahili wako na clans kwa mfano kwa Wakilindini kuna Mwenyenguti wa Mwenyesaidi au Mwenyenguti wa Mwesangu, kuna Mwenyeshoka upande wa Wawakilifi, haya mambo tungependa katika Katiba ya Kenya yasisitize na wakati kukiletwa watu kuandikisha watu hapa kuhusu makabila sehemu hii wawe ni watu ambao wanauzoovu mzuriwa watu wa sehemu hii. Kusiletwe mtu ambaye ukimuambia mimi ni Mkilindini akuambia hakuna kitu kama hiyo. Jambo jingine ambalo pia ningependa kuisitiza Tume kuna sheria nafikiri mwajua ya kwamba mashirika yote ya serikali na yasio ya serikali yanapombuni au kufungua ofisi kwenye sehemu yoyote nchi ya Kenya ni sheria lazima asilimia themanini na tano ya wafanyi kazi kenye mashirika hayo yawe ni wenyeji wenyewe. Jambo la kusikitisha nchini Kenya sehemu zote zinatekeleza sheria hii isipokuwa sehemu ya Pwani.

Tukija kwa upande wa Kilindini Port, kufikia mwaka elfu moja tisa mia na sitini, kulingana na stationary paper number number 9 ya 1961, Kilindini Port kwa Kenya koloni na Uganda exports and imports ilikuwa inaingiza total ya million pound zaKiingereza mia moja na sabini na moja. Ni jambo la kushangaza sana kuwa pesa zinazolingia kupitia kilindini na mambo ya tourism hatujaonyeshwa hesabu zake zinavyotufaa sisi kiwango ya kwamba tuko na shida sana mpaka ya maji ya kunywa.

Health care dawa kwenye mahospitali yetu Pwani hakuna. Ardhi kwa wa pwani limefikia kiwango ya kuwa wanaishi kama ma-squatter licha ya kuwa iko historia ya watu kama Wahindi, Waarabu walikuweco hapa kabla ya watu wengi ambao sasa hivi wanajiita wananchi wa Kenya. Kwa mfano 1497 Mhindi anajiita Ahmed Madida anapeleka Vasco-Dagama Calcata. Huu mnazi unatoka Gujarat miaka elfu mbili na mia tano iliyopita. Mhindi huyu ambaye ameishi hapa kwa umri huo unawezaje kusema si Mkenya. Mwarabu ambaye yuko kutoka kuandikwe preference of the Iretrian Sea unaweza kusema si Mkenya

mpaka alae birth certificate ya nyanya yake na babu yake anapotaka birth certificate or ID, wakiti ambapo akija babu yake na nyanya yake hata Mwingereza aliyoleta birth certificate na ID alikuwa hajakuja kutawala.

Wazee wangu na ndugu zangu na maCommissioner mliokuja hapa nimekuja kuongea na nyinyi kwa ufupi kwa sababu dakika mnazotupa hazitutoshi lakini hata hivyo tutafuata sheria, Tumesema haya machache na mengi zaidi tutakwenda sehemu nyingine tutakuja kujieleza zaidi na kutoa ushahidi. Lakini ninasisitiza tena, nataka kwa isani zenu ikiwezekana mkataba uno mtutekelezee ardhi zetu zilizonyakuliwa tangu uhuru na hata ikiwezekana kabla ya uhuru zirudishwe kwa wenyeji. Mbali na hayo tunaomba kutoka leo wanaosimamia serikali wasipuuze tena sehemu ino kwa sababu kama tulikuwa Tumelala kama tunaomba kutoka leo wanaosimamia serikali wasipuuze tena sehemu ino kwa sababu kama tulikuwa Tumelala kama

Tatu, wajumbe wetu kwenye Bunge hawajasema lolote kuhusu mikataba ino aidha kwa kuwa hawajui au waogopa. Kwenye kifungu cha kwanza ni uhuru wa ibada, kifungu cha tano ni kuhusu haki za kumiliki ardhi yasiopaswa kulipa kodi. Free hold titles baada ya Kenya kupata uhuru wenye free hold titles walipuuzwa na wakatozwa kodi na serikali na hii ni kinyume cha mkataba uno baina ya Kenya na wenyeji halisi wa sehemu ino. Kwa maana ino tungependelea zaidi mkataba uno nyinyi ma Commissioners muutie maanani na muhakikishe:-

- (d) Kenya imetueleza kwa nini imepuuza.
- (e) Baada ya kuupuzwa afari ambayo imetupita wenyeji wa sehemu ino, Kenya itairekebisha na kutulipa vipi?
- (f) Waakikishe mkataba uno umetekelezwa kama ipasavyio.

Tunakuja kwenye Wakfu commssion. Kama alivyoeleza ndugu yangu Sheikh Halifah ino ni hazina ya Waislamu lakini kutokana na Wakfu Commissioners Act Chapter 109 inatoa ruhusa ya kubuniwa, to establish an independent body ambayo ina watu wannane. Katika watu wanane hawa wote ni appointees wa serikali na wakichaguliwa wanaenda kwa PC yeyote wa Pwani, PC atawapeleka kwa Attorney General, Attorney General atawaidhinisha. Mjadala huu tunaupinga kwa sababu PC wa Pwani na Attorney General kisheria ya dini yetu hawaruhusiwi kusimamia pesa zetu.

Tunakuja kwenye appointment ya Chief Kadhi, natumaye ma Commissioner nyote mnajua kwamba Chief Kadhi nchini Kenya anachaguliwa na Judicial Service Commission. Kwa maana ino nitakuwa nafikiri si kukosea nikisema chief Kadhi ni:- (a) mfanyi kazi wa serikali (b) anawakilisha serikali kwenye jamii ya Waislamu kuhusu maswala ya dini ya Islamu na Waislamu wenyewe. Kinyume na sheria za dini ya Islamu, Chief Kadhi anatakikana awe ni msimamizi wa sheria na mamlaka ya dini ya Islamu awakilishe Waislamu kwenye serikali. Kwa maana ino ningepomba pia Tume ino isisitize kwenye Katiba kuwa Chief Kadhi iwe hatachaguliwa na serikali na yuapo atachaguliwa na serikali sisi tutakuwa hatumutambui.

Kuhusu ndugu yangu hapa ambaye amewakilisha disabled, ningependa kuisitiza Tume kama itilie maanani sana kuwasaidia walemavu wa aina tofauti, wawe ni wanawake au ni wananume , waweze kuwabunia na kuendeleza infrastructure yao kwa mfano mabasi ambao watakuwa wanapanda wao peke yao na vituo vingine vya huduma tofauti ambavyo vitakuwa ni vya wasio

jiweza. Hili ndio ningependa kuisitiza kwa niaba ya walemavu.

Tukija kwenye issue ya Waswahili ambao Ni wenyeji halisi wa sehemu ino ya mwamba wa pwani, mimi mwenyewe wakati nilipokuwa nataka kuchukua kitambulisho nilipingana sana na ma clerk au makarani waliokuwa wakiandikisha kwa kutaka kunilazimisha niitwe Swahili Shirazi. Waswahili waheshimiwa hapa wako makabila kumi na mbili, makabila haya yako kwa tabaka kwa mfano kuna Wagunya, Wafaza, Wafafi, Wakatwa, Washaka, Wakilifi, Wamtwapa, Wamvita, Wakilindini, Wachangamwe, Watangana, na Wanjoni. Bali ya kuwa katika kabila Waswahili wako na clans kwa mfano kwa Wakilindini kuna Mwenyenguti wa Mwenyesaidi au Mwenyenguti wa Mwesangu, kuna Mwenyeshoka upande wa Wawakilifi, haya mambo tungependa katika Katiba ya Kenya yasisitize na wakati kukiletwa watu kuandikisha watu hapa kuhusu makabila sehemu hii wawe ni watu ambao wanauzoevu mzuriwa watu wa sehemu hii. Kusiletwe mtu ambaye ukimuambia mimi ni Mkilindini akuambia hakuna kitu kama hiyo. Jambo jingine ambalo pia ningependa kuisitiza Tume kuna sheria nafikiri mwajjua ya kwamba mashirika yote ya serikali na yasio ya serikali yanapombuni au kufungua ofisi kwenye sehemu yoyote nchi ya Kenya ni sheria lazima asilimia themanini na tano ya wafanyi kazi kenye mashirika hayo yawe ni wenyeji wenyewe. Jambo la kusikitisha nchini Kenya sehemu zote zinatekeleza sheria hii isipokuwa sehemu ya Pwani.

Tukija kwa upande wa Kilindini Port, kufikia mwaka elfu moja tisa mia na sitini, kulingana na stationary paper number number 9 ya 1961, Kilindini Port kwa Kenya koloni na Uganda exports and imports ilikuwa inaingiza total ya million pound zaKiingereza mia moja na sabini na moja. Ni jambo la kushangaza sana kuwa pesa zinazolingia kupitia kilindini na mambo ya tourism hatujaonyeshwa hesabu zake zinavyotufaa sisi kiwango ya kwamba tuko na shida sana mpaka ya maji ya kunywa.

Health care dawa kwenye mahospitali yetu Pwani hakuna. Ardhi kwa wa pwani limefikia kiwango ya kuwa wanaishi kama ma-squatter licha ya kuwa iko historia ya watu kama Wahindi, Waarabu walikuweco hapa kabla ya watu wengi ambao sasa hivi wanajiita wananchi wa Kenya. Kwa mfano 1497 Mhindi anajiita Ahmed Madida anapeleka Vasco-Dagama Calcata. Huu mnazi unatoka Gujarat miaka elfu mbili na mia tano iliyopita. Mhindi huyu ambaye ameishi hapa kwa umri huo unawezaje kusema si Mkenya. Mwarabu ambaye yuko kutoka kuandikwe preference of the Iretrian Sea unaweza kusema si Mkenya mpaka alaete birth certificate ya nyanya yake na babu yake anapotaka birth certificate or ID, wakiti ambapo akija babu yake na nyanya yake hata Mwingereza aliyoleta birth certificate na ID alikuwa hajakuja kutawala.

Wazee wangu na ndugu zangu na maCommissioner mliokuja hapa nimekuja kuongea na nyinyi kwa ufupi kwa sababu dakika mnazotupa hazitutoshi lakini hata hivyo tutafuata sheria, Tumesema haya machache na mengi zaidi tutakwenda sehemu nyingine tutakuja kujieleza zaidi na kutoa ushahidi. Lakini ninasisitiza tena, nataka kwa isani zenu ikiwezekana mkataba uno mtutekelezee ardhi zetu zilizonyakuliwa tangu uhuru na hata ikiwezekana kabla ya uhuru zirudishwe kwa wenyeji. Mbali na hayo tunaomba kutoka leo wanaosimamia serikali wasipuuzie tena sehemu ino kwa sababu kama tulikuwa Tumelala kama tunaomba kutoka leo wanaosimamia serikali wasipuuzie tena sehemu ino kwa sababu kama tulikuwa Tumelala kama tunapoambiwa tunaongoja maembe safari hii Tumeamka na maembe tutayakula hata yakiwa mabichi. Na kufikia hapo nashukuru asanteni sana nyote

madugu zangu na wazee wangu asanteni nyote.

Com Salome: Asante sana Bwana Stabul. Kuna swali kwa bwana Stabul. Margaret Mbaya.

Margaret Kasichana Mbaya: Habari zenu? Hapa nimekuja mna maoni yale yangu ambayo niko nayo. Majina yangu ninaitwa Margaret Kasichana Mbaya. Jambo la kwanza ambao nimeona nilete hapa ni kuhusu haki za kina mama, nimeandika kwa ufupi kwamba haki ya kina mama zitekelezwe. Mfano kama mama ameolewa upande wa kule kwa baba na mama alipozaliwa kama kuna uradhi wa watoto isiwe tu kwa watoto wa kiume bali wapewe hata wale watoto wa kike waliolewa kwa maboma mengine.

Ya pili ni kuhusu chokora, serikali ningeopmba hawa chokora badala wasumbue watu na wageni wetu wa watalii wanaotoka mbali kuja kutembelea nchi yetu watafutiwe mahali kama vile hizi miji zingine za watoto. Wajengewe mahali hata kama ni kando na wapatiwe vyakula na nguo na wasomeshwe. Haya ningependa kusistiza hii ingine ya ma polisi, mapolisi hata jana pale, yaani mtu atakayeshuka katika ile stage ya Njisi, Tayari unaambiwa kuja hapa mama ama kuja hapa mtoto ama baba, kwa ma baba na ma mama ni afadhali lakini kwa watoto hata wa skuli hiyo ndio tunasikitika sana kwa sababu hata akiwekwa pale inaonekana mtoto ameketishwa hana hata ndururu anatoka pengine kwa mama yake ama kwa nyanya ya ke kutembea tu akirudi kwa anakalishwa na hana la kusema na hana mobile ya kupiga nyumbani kwao na kwao hakuna mobile sasa ni mpaka aende kule kama ni Mapuva ama ni wapi. Halafu siku hiyo akipelekwa huko ama siku ya pili ama ameshikwa Ijumaa mpaka Monday aende kotini, akienda kotini mambo ni mapesa na watu hawana pesa. Unaambiwa elfu mbili na hiyo ya chakula mwenyewe pia hauna. Mimi kwa ufupi ni hapo hapo.

Com Salome : Asante sana Margret Mbaya. Kuna swali kwa mama Mbaya.

Speaker : (inaudible).

Com Salome: Asante sana kwa swali lako, hilo ni swali la mjadala.

Margaret Kasichana Mbaya: Haina haja ajibiwe? Asante sana.

Com Salome: Tafadhali Tumepe nafasi mama Maggie Gona, karibu.

Maggie Gona: Asante. Commissioners nyote nawasalimu na ninawaambia karibuni Pwani. Wapwani wezangu, mabibi na mabwana Salama maleku. Nataka kuhakikisha kwamba twashukuru kina mama wame-play a big part in raising the standard of Kenya kabla ya uhuru na baada ya uhuru. Kwa upande ya kimaendeleo nafikiri sisi tuko number one. Si kila mtu ananijua mimi

ni Maggie Gonna? Halafu nani anauliza tena. Mimi ni Maggie Gonna.

Lakini tukiangalia katika halumu ya kimaendeleo kwa jumla Kenya women have been marginalized. Yaani Tumerudishwa nyuma, hatuonekani popote na mambo kama hayo particularly kina mama wa Pwani kwa jumla.

Kwa upande wa gender issue ni kama nilivyosema na ninasistiza kwamba tuwe tutapewa nafasi ya kila upande kwa upande wa kiserikali, policy making institutions zote na hata kwa mfano kama kuna wengine kina mama waliochaguliwa. Nimeshasema mambo ya gender ya kwamba kina mama mpaka sasa kina mama Tumewekwa nyuma hasa kina mama wa Pwani. Nikisema hivi ninazungumza kwa upande wa policy making institutions na vetting ya institutions kama Parastatals bodies and so forth. Hapa Pwani Tumebarikiwa kwa kuwa tuna Parastatals nyinyi kama vile KTDA tulikuwa na vile vile na Kenya Cash nuts sasa ishakufa lakini hatujui itafufuka lini lakini Inshall kwa uwezo wa Mungu itafufuka. Hapo hakuna hata mwanamke mmoja hasa mwanamke wa Kipwani. Kwa hivyo kwa jumla Constitution ningependa kiwango hiki kikiwe ya kusema kabisa kusiwe na ubaguzi kati ya waume na wake, we are all human beings and we should be treated accordingly.

Kwa upande wa citizenship katika station thamanini na tisa mpaka tisaini na mbili and I quote, “for the Constitution this should be amended to remove the gender double standards that reduce women to second class citizen and privileges Kenya’s women citizen right over those Kenyan women”.

Kwa upande wa mambo ya sheria family law the provision or the affiliation Act should be re-introduced through the Constitution.

Kwa upande.. kuna shida gani. The new Constitution should provide and protect the transformation of Kenya society from being largely paralyzed and assist us economy and industrialise us.

Customary laws, sisi watu wa Pwani nafikiri tuna desturi zetu ambazo tunataka desturi hizo ifadhiwe ikiwa zinahusu dini yetu ya Kiislamu lazima zihifadhiwe kwa ajili ya Korahani inavyotwendesha. Tusiwe na mabadiliko yoyote na ikiwa kuna mabadiliko yoyote kwa mfano kama ni upande wa Muslim Law watu wanaohusika katika Muslimwao wawe wataanasishwa na ikiwa ni lazima kugeuzwa basi itakuwa ni haki yua wenyewe kwamba jambo hili ndilo litatekeleza.

Constitution vile vile ni lazima iwe amended to allow for independent candidates in civic, parliament and presidential elections. Nikisema hivi nikizungumza habari ya democracy eh! Mimi pengine niko KANU ma niko DP nasikia kila mahali, pengine nilikuwa nataka nisimame lakini kuna mwingine ambaye atasimama. Sasa kwa nini, iwe independent mtu mwingine apate nafasi mwenyewe, haya basi mume na nguvuzi.

The Constitution should also provide the right to access information, right to civic education and right of legal education.

Mambo ya lugha ambao tutaitumia katika Katiba yetu ni furaha yetu sisi kuona kabisa kwamba Katiba hiyo imeandikwa kinaganaga, tunajua kuna vile lawyers language. Wengi sisi sio ma lawyer wala hatuna haja ya kuwa lawyers kwa kuwa we are satisfied with what we are. Iandikwe katika lugha ambayo ordinary mwananchi ataelewa.

Kwa upande wa affirmative action mimi ningesea tu kabisa kwamba matakwa ya kina mama lazima yatimizwe. Kuna nafasi nyingi sana zimetokea lakini twanyimwa, twanyanyaswa hata katika parliament nominated members kuna special seats za kina mama. Leo utaona mwanamume ndio ametiwa just because he belongs to abcd. Hiyo ikiwa ni nafsi yetu kina mama na lazima itive katika Katiba wazi ionekane.

Kwa upande wa culture ni kama nilivyosema sisi wa Pwani tuko tofauti na wa Bara maana ikiwa kuna mtu wowote wa Bara hapa atanisamehe lakini ukweli lazima usemwe. Culture ya watu wa Pwani ni tofauti na ya wa Bara na culture hiyo ni lazima I we itaudumiwa vilivyo. Na nikisema culture hiyo ni kwamba hebu ni seme Commissioners kwamba hapa kwetu Pwani hakuna Mwarabu timamu. Utasikia huyu ni Mwarabu kumbe mama yake ni Mgiriamu, na mimi nasema wazi kabisa kwamba hata katika usalama sisi tulikuwa hatujui kuiba, hatujui kufanya hivi na hivi Tumefundishwa na hawa wa Bara lakini culture yetu nataka hiyo kitu iingizwe kwa Katiba, culture ya watu wa Pwani na tusibaguliwe kwa chochote. Mkate wa keki unakuja Kenya nzima ukitoka popote unapotoka keki hiyo hatutaki ibakie huko sisi pia we are part and parcel of this country and we should enjoy all privileges whatever it is.

Kidogo Kenya yetu Tumesahau walemavu, ningependa kabisa kwamba disability persons wale ambao hawajiwezi wafikiwi vilivyo na iwe imeandikwa katika Constitution yetu kinagaga tutawafanyia nini wapate haki zao.

Mambo ya Kadhi courts sipendi kuyasema sana maanake I am not qualified on that lakini ninaunga mkono maneno yaliyotolewa na bwana Halifa. Hayo nataka yaingizwe ndio kina mama pia tunasema lazima mambo ya Kadhi. Na hata hivyo you know we are on a changing society, ningefurahi vile vile hiyo kadhis court tuwe vile vile tusiwe na kina baba peke yake. Kina mama lazima wawe katika kadhis court maanake mimi ni rahisi kuzungumza shida zangu na mke mwezangu zaidi ya mwanamume. Mimi nitamuambia nini bwana Hamisi, lakini naweza kumuambia Rubeda Sumba maneno mazuri sana, ile shida yangu. Kwa hivyo katika hizi court ambazo ni lazima za kuhudumiwa tuone kuna women's desk. Na women's desk wasikuwe wakaa ah! Awe na power ya kusema ukweli na ataka nini kwa kina mama. Tumenyanyaswa sana na sitaki jambo hilo liendelee.

Mwisho Commissioners asanteni kwa kufika lakini mtu anataka kusema kabisa kwamba Pwani kwa jumla tuko imara kwa maendeleo yetu ijapokuwa tunalaumiwa ati kwamba twangija maembe, maembe ni yetu na tutakula leo na kesho. Watu waenze kufikiria maembe, tutaendelea kula maembe lakini tunataka humanity, ile human rights iwe itasimamishwa kabisa vizuri na tupate haki zetu kwa ajili ya Mungu mwenyewe alivyopanga. Asante kwa nafasi hiyo.

Com Salome: Asante sana mama Maggie Gonna. Kuna swali kwa mama Gonna. Sasa ningetaka kumpa hii nafasi kwa

mwenyekiti wa KANU mvita branch.

Simon Rojas: Makomishona mliokuja kwanza ninawaamukua hamjambo? Mimi ninayezungumza ninaitwa Simon Rojas Musech. Kwa ujuzi Mungu alinipa na kwa umri Mungu alionipa nataka niwaambie maneno ambayo....

Com Salome: Umejita mbua kwa majina?

Simon Rojas Musech: Ninaitwa Simon Rojas David Musech, Chairman wa Mvita wa KANU. Mimi nilikuwa ndio senator wa kwanza Mombassa hii, mimi nimeitumikia council ya Mombassa kwa miaka kumi lakini nataka kuzungumza ni kwa nini nilikuwa senator, watu wengi hawajui hayo, wengine wamezaliwa siku za juzi. Mambo ya senator ilikuja kwa sababu tulikuwa na Katiba ya nyumba mbili, tulikuwa na Upper House, Lower House, tulikuwa na Regular Assembly na local council.

Com Salome: Nataka kuwaomba msipige makelele ili tuwe kumpata.

Simon Rojas Musech: Narudi tena hapo hapo. Asili ya mimi kuwa senator 1963-1965 ni kwa sababu Katiba ya Kenya ilikuwa inaruhusu Kenya iendeshwe kimajimbo, na kimajimbo ilikuwa ni Upper House, Lower House, Regional Assembly na Local Councils. Watu wakipiga kura nne. Katiba hiyo Tumekwenda nayo lakini kwasababu wa Kenya wengine hawataki wenzao waende kisawasawa wakaibadilisha Katiba na ilibadilishwa si kwa sababu ilikuwa mbovu, ilibadilishwa kwa shabaa ya watu fulani maalum walikuwa na tamaa, wengine Mungu ashawajibu washakwenda mbele ya Mungu, wengine bado wangali wako hai, wengine ni sisi ambao tulipinga mpaka mwisho. Kwa nini Katiba ibadilishwe na ambapo inatufaa. Kwa hivyo mimi naona leo Kenya tena inarudia history, watu wanataka majimbo. Basi kwa sababu ya kutaka majimbo, makomishona tuelewane, hii sababu ya kutaka majimbo si sababu tu ya kutaka majimbo ni kwa sababu watu wamenyanyaswa Coast ikiwa number one, watu wa Pwani wamenyanyaswa na kila utawala. Utawala wa Mreno, utawala wa Mwarabu, utawala wa Mzungu, utawala wa Kenyatta na leo ni wa Moi. Kwa hivyo Katiba hii tikiimba majimbo hatuimbi kwa sababu ati ni sharti ya kuvaa, twataka majimbo haki zetu ziwepo hawa watambuliwe, kubaguana kuishe, kwa sababu leo Mombassa huwezi kuniambia huyu ni Mwarabu, mimi naweza kukataa. Kwa sababu pengine mamake pengine, ama nyanya yake alizaa na baba yangu. Kwa hivyo hapa Mombassa na Pwani nzima kwa jumla tuko tofauti sana na wa Kenya wenzetu kule. Wakenya wetu wahesabu president ni yule waziri wangu ni yule, Mbunge wangu ni yule, elimu yangu ni hapa, hakuna njia ingine inayompatia taabu. Sisi twahesabu ukiamka asubui kibarua nitapata wapi, leo nitakwenda kwa nani kwa taabu zilizoko. Kwa hivyo Katiba hii tafadhali, it is not a joke, this is very serious. Kwa sababu Kenya chini ya ki-Africa imekuwa pia na classifications. Huyu ni wa huyu, huyu ni wa yule tutaishi vipi. Kwa hivyo wakati tunakuja tunajua this is the last time, mimi nina experience ya kutosha, Katiba haishi leo na hakuna Mkenya aliye tayari.

Elections isifanywe kwa Katiba hii mbovu, twataka Katiba hii mnayotengeneza. Ikiwa waliikataa kwamba ni mbaya, kwa nini tufanye elections nusu nusu. Why, tupate klatiba ya sawa sawa na Katiba tafadhali msiharakishwe. By experience hata

mkamaliza mwezi wa March you need another 6 months to satisfy the Constitution of this country. Kwa hivyo msilale tu election, Oh nataka kumchagua ndugu yangu, nataka kumchagua shangazi, hapana, tulale Katiba iishe iliyo safi inayofaa Wananchi wa Kenya. Ma Commissioner hii karatasi yangu ina mambo kidogo hapa lakini nitawapa na hii ni ya tatu. Wimbo ni ule ule, sijabadilisha. Mlipokuja mara ya kwanza tukawapa, mkaja mara ya pili tukawapa leo twawapa ya tatu, ngoma ni kile ile dawa ni majimbo. Na majimbo yatiwe nguvu kwa sababu ikiwa hamjui kwa sababu katika Kenya there is a political fear among the community this is bringing about all this things. One:- classification of human beings, we are Africans but we are classifying ourselves. Kwa nini? Vile vile ukienda kuongea na Mwaamerika, hakuambi mimi ni mwa Afrika mimi natoka Nigeria. Aha! Akuambia ni mwa Merika. Sisi hapa Oh! Huyu ni mwarabu huyu ni Mbunya huyu, huyu ni Mbunya huyu, huyu ni Mtaita, huyu ni Mgiriama. Yajiani haya yote, ni Kwa sababu ya taabu zilizoko. Hii ndio ugonjwa ulioko. Kama mkiweza kutia humu ndani kwa Katiba hii mjui haki ya kila Mkenya, mjue haki ya kila mama. Hapa kumesemwa maneno mengi sana hapa, ijue haki wasiojiweza, ijue haki ya masikini. Marehemu Nyerere alisema nyinyi wa Tanzania mnapiga kelele hapa, watu wengine wako Kilimanjaro wengine wako Mbale, tutapatana lini, sidhani kabisa. Hii maanake watu wengine they are too high, they are too rich. When is the poor going to come up or will they stay like that. Hii gap ni kubwa sana, elimu yako ya bure haikusaidii kwa sababu family yako yote ni masikini, elimu yako haifai. Kwa hivyo ma- Commissioner mimi nimesema muundo wa serikali uwe na mfumo wa majimbo halafu ma/kamu wa raisi himo katika hiyo, sitaki kusoma yale yalioko chini ya hayo.

Halafu waziri Mkuu, halafu manaibu wa waziri wawili, halafu Baraza wa mawaziri na anayepaswa kuwa traia wa Kenya, hii imeshazungumzwa hapa, wale walizungumza ni kama walikuwa pamoja na mimi.

Vyama vya siasa, mpangilio wa uchaguzi, haki za aridhi na mali, na mwisho nifikayo. Kwa hivyo aliye na swali aniulize sina mengi karatasi nitapeleka pale.

Abdula Ali: Salama maleku. Jina langu ni Fadhili Abdulamani Ali na nimetoka katika kikundu cha Bidhaa Environment Group na nimekuja leo kutoa maoni yangu kidogo hapa.

Kwanza nimependa kutoa maoni kuhusu Katiba yetu tulionao hivi sasa. Shauri Katiba inayoendelea hivi sasa ni karibu vifungu vyote ni za kikoloni. Kwa hivyo tunaiomba Tume hii ichukulie sana mjadala huu kuitilia chini na hii Katiba ifutwe kabisa kikoloni. It means kwamba Katiba ambao iko iliotunga hii Sheria ambao ndio inatutawala hivi sasa. Kwa mfano Sheria ya chifu hiyo ni Sheria moja ya kikoloni, na Sheria ya msako hii kusaka mwananchi wa Kenya wakati yuko ndani ya nchi yake hiyo ni Sheria kubwa sana ya kikoloni. Maanake mkoloni aliweka Sheria ya msako kwa manufaa yake mwenyewe ili mwafirika asiweze kuwa na haki.

Tatu ni Sheria ya trespass, hakuna mtu yeyote anayekanyaga land ya Kenya kwamba yuko nje ya Kenya. Sasa wewe utakanyaga land ya Kenya halafu tena uambiwe tress pass, hii tayari ni ukoloni mambo leo. Sheria ya ardhi, kwa mfano Sheria ya aridhi ilitungwa 1915, wakati huo 1915 sheria hii ya ardhi ilikuwa imetungwa kwa niamba ya mkoloni ili mwa- Afrika asipate

haki ya kumiliki aridhi. Sasa kwa hiyo tunaona Sheria hii ya kifungu ishirini na nane ingebadilishwa, naona ingebadilishwa ikabidi apewe Mwafrika nguvu ya kuweza kutawala aridhi yake sawa sawa.

Sheria ya kuwa uhuru wa kwenu, kwa sababu saa hii wa Kenya tuna uhuru lakini uhuru wa kikweli hatuna. Unaona. Maanake Mkenya saa hizi bana kuna mambo mengi sana ambao tunazuiwa kwa ajili ya quality. Quality yako ikionekana wewe ni black basi hutaipata kihaki. Sasa kwa hiyo hiyo nafikiri ingekuwa mmoja yapo kilichotolewa na kuwa na uhuru ya kisawa sawa yaani kila mahali unapokwenda unafanyiwa kazi yako, kama ni kwa ofisi wapi wanakushugulikia kwa uhakika kama raia wa nchi.

Ingingine ni kuweza kuchangia maoni kwa Wananchi, unajua mpaka sasa hivi lkuna Wananchi wengi sana wana maoni mazuri ambao wanaweza kusaidia katika serikali, nyanja mbali mbali kama vile Mbungeni, mpaka kwenye Baraza ya Majiji. Kwa hivyo ilikuwa inabidi kwamba kama ingewezekana, ingekuwa raia pia wanaruhusiwa kutoa maoni yao katika mabaraza ama Bungeni. Especially hata kama ingekuwa wanatoka katika vikundi fulani ya Maendeleo kama ya kina mama au Youth Group ambao ingeweza kuchaguliwa at least hata representative wawili au mmoja ambao angeweza kukaa katika kikao either cha Baraza ama cha Bungeni naye ajadili kutokana na mawazo ya watu wao alikotoka community yao.

Ingingine ni elimu; Tumesoma sana katika vitabu vingi kwamba sera zetu au agenda zetu zilizokuwa za wakati wa kupigania uhuru, agenda yetu iliokuwa kwamba baada ya uhuru kunyakuwa elimu ikakuwa bure. Baada tu ya kunyakuwa uhuru ile elimu iwe bure lakini tunashangaa mpaka hivi sasa elimu imekuwa ghali sana mpaka kiwango masiki wa kawaida hawezi kumsomesha mtoto wake. Ijapokuwa tunalipa kodo haina mbali mbali zote ambazo zingeweza kuchangia kuwa na elimu ya bure katika nchi yetu. Kwa hivyo hiyo ni muhimu sana, ijadiliwe kwenye kikao irudishwe elimu ya bure kwa Wananchi.

Swala ingine ni kumiliki mali ya asili; nafikiri nchi yetu all over kila mahali kuna mali yake ya asili katika Kenya nzima unakuta kuna mali ya asili ambaye tunaweza kuitumia sisi wa Kenya kuinulia uchumi kwa sababu hivi sasa uchumi wetu umeanguaka kabisa. Sasa nafikiri kama kungekuwa na Katiba ambayo ingekuwa inamruhusu Mkenya kutumia mali ya asili yake ya nchi yake, kwa mfano kama vile madili. Uvuvi wa baharini maswala aina mbali mbali ambao katika mali asili inaweza kutuiniulia sisi uchumi. Mali ya asili zote zimekupatiwa tu na watu ful;ani na nusu zimekaa katika serikali. Saa zingine mali asili kama nchi zingine jirani mfano tunaona Tanzania, Wananchi wamepewa haki ya kuchimba madili yao, kufufulia uchumi wao maanake uchumi umesorota. Uchumi bado umesorota na mali asili ni yetu, kwa ninji Wananchi wasipewe vibali, mtu avue bure. Saa hii mtu mvuvi akienda kuvua anakamatwa tu anawekwa ndani na wakati anavua bahari ya Kenya. Sasa aende akavue wapi? Bahari ya Uganda au wapi?

Halafu jambo lingine amabla la weza kuwa la mwisho ni sera za majimbo. Sababu Tumeona tangu Kenya hii ipate uhuru, serikali kuu imeshidwa kutekeleza wajibu wake. Tumeona ubaguzi wa kimikoa miaka thelathini na nane. Kwa hivyo ninatoa maoni kwamba serikali itakayo kuja itilie maanani maswala ya majimbo. Wananchi Tumechoka na serikali ya katikati, twataka jimbo. Kila jimbo limiliki mali yake. Tunataka serikali itakaokuwa kila mkoa tutatumia rasilimali yake haswa. Si majimbo ni

swala la kufukuza mtu! Sote ni watu wa moja wa Kenya lakini swala la majimo ni zile kumiliki mali za pale. Kwa mfano tukiangalia kama Kisumu, Kisumu ni sehemu ambayo ina ziwa Victoria, ina ukulima kule wa pamba, kuna mambo mengi sana ambao yaweza kufanya ile nchi iendelee na mikoa mingineo yote. Lakini unakuta kulingana na serikali kuu, pesa yote inayokuja kutoka either nje ama pesa ambayo imepatikana ndani ya nchi inakimbilia tu sehemu moja halafu sehemu hiyo ndio inakuwa inanufaika na pesa za mikoa yote. Sasa unakuta mikoa mingine inaanguka. Lakini iwapo tutapewa mueleo mzuri, kila mkoa uweze kufanya miradi yake, it means kwamba hatutakuwa na ubaguzi wowote. Asanteni sana sina zaidi ya hapo.

Speaker: (anauliza swali) inaudible.

Abdula Ali: Okay mzee wangu nimeshukuru kwa hiyo swali ulioliza. Unajua wakati inapofikia kwamba tuchague polisi kuwapeleka Kiganjo wakafundishwe uwa ni sawa sawa umjechukua mtoto kumpeleka chuoni kumfudisha Buruani. Sasa ukimchukua mtoto wa chuoni aliyetimu halafu umpeleke kwenye hetima aseme hajui kusoma itakuwa jambo la kuchekesha. Sasa wakati polisi wanapopeleka kiganjo uwa wanapeleka kufunzwa mafunzo yana hitilamu, mafunzo ya kumuangalia mtu na kumjua huyu ni nani, au mafunzo ya kuangalia mtu njia navyofikiria. Sababu uwezi kufanya msako kila mtu wowote kaa nchini, wewe kaa chini hapo utakuwa husaki mwizi. Mwizi unaweza kumuona kwa vitendo au ukimuona kwa njia zake na vile anaringa ringa manyumba ana mipango fulani fulani unajua huyusi raia mwema. Lakini iwapo raia mwema anatembea kwa mfano kama hapa kwetu Mombasa tunapoonika ikifika Ijumaa na Jumamosi ni kama polisi wanajua ufisadi ni kuwashika watu mitaani na kuwatoa mapeni. Na mambo tushapeleka mpaka kwa Mkubwa anajua haya. Kwa hivyo wana ujuzi isipokuwa wanafanya kusudi.

Com Salome: Asante sana. Ninaombwa kupatia hii nafasi kwa ndugu zetu wenye ulemavu wenye wameingia lakini tayari hata hawajaweza kuketi waka... angaa wakapata kufikiria kama wangetaka kuzungumza ama laa. Kwa hivyo nitaanza nao leo alasiri na wakati huu nitampa bwana Seif Ali.

Seif Ali Mohammed: Mimi jina langu ni Seif Ali Mohammed natoka hapa Mombasa Kisauni na kwanza ninawashukuru ma-Commissioner wote na wanawake na Wanaume. Salama maleku?

Maoni yangu ya leo ni kwanza mfumo wa serikali mimi napendelea kwa maoni ya/ngu iwe mfumo wa majimbo kama ndugu zangu wengine waliota/ngulia. Hii ndio itakayo kuwa suluhisho kwa wa Kenya wote. Bila hiyo hakuna suluhisho, wakipenda wasipende. Ndugu zetu walioko hapa wa bara, wakipenda wasipende suluhisho la hii Kenya iwe mzuri na iwe Kenya moja ni iwe na serikali hizo za majimbo.

Ya pili, tunataka watoto wetu wote kuanzia primary level wafundishwe elimu ya kutambua haki zao na hii elimu wafundishwe mpaka wafikie huko university kuanzia hapo chini. Hatutaki mtoto mjinga katika Kenya asiyejua haki yake, iandikwe hiyo kwenye Katiba, kila mwanafunzi anayetoka Kenya, anayetoka Kenya mzaliwa apate hiyo mafunzo, atambue haki zake za

kikatiba zote kwa jumla.

Iwepo nafasi kwa kila jimbo, kila Mkenya apewe nafasi yake kutoka jimbo yake haki yake ya kwanza kabisa. Haki yake iwe ya msingi atapewa kila Mkenya pale alipo katika jimbo lake, elimu ya bure, maji ya bure, matibabu ya bure, apewe kila Mkenya pale alipo katika jimbo lake. Ingingine, haki ya msingi, apewe uhuru wa kujiamulia mambo yake, afanye vile yeye anaona ni sawa kwake na iwe sawa kwa wenzake.

Nyingine haki ya Mkenya, ikiwa anataka wadhifa wowote, ikiwa ni diwani, awe na elimu ya kiwango cha 'O' level au zaidi. awe ni mwana siasa wa kuzaliwa, sio wa kubadikwa, awe ni mchangamfu, aweze kuwaelewa watu wake na watu wake wamuelewe yeye ni nani. Na yeye awe anatoka pale pahali anaposimamia wadhifa wowote ule anautaka. Ikiwa ni udiwani ikiwa ni Mbunge, wadhifa ule awe amejitolea kusimamia pale mahali kwao alipozaliwa sio atoke mahali kwingine aende akasimamie watu ambao hawajui. Wadhifa huo inatakikana mtu awe na elimu. Kwa hivyo tunaomba ikiwa ni Mbunge awe na elimu ya degreefulani, awe na degree ama awe na diploma lakini awe na kiwango cha elimu ya kutosha kuwaudumia watu wake ipasavyo. Na yeye mwenyewe awe atakuwa ana wajibika katika kazi zake hizo zote. Ikiwa ni diwani, awajibike katika kazi zake zote, akiwa ni Mbunge, awajibike katika kazi zake hizo za ubunge. Akiwa ni raisi kadhalika awajibike katika kazi zake za uraisi na hatutaki kiongozi yoyote awe juu ya Sheria. Kila kiongozi awe chini ya Sheria, anayefanya kosa ahukumwiwe na mahakama kama Mkenya mwingine yoyote wa kawaida. Kuwe na haki kwa watu wote kusiwe na ubaguzi, huyu ni mwanamke, huyu ni mwanamme, wote wawe sawa kuhudumiwa. Katika ugawanyaji madaraka,. Madaraka yapewe kila Mkenya, ikiwezekana raisi atoke kila jimbo kwa muhula kwa kipindi, kipindi hiki cha miaka mitano raisi alitoka Rift Valley ni Mnadi, kipindi chengine atoke Nyanza, Mjalu kwa zamu. Ikiwa ni Muislamu safari nyingine awe Mkristo lakini atoke jimbo jingine. Kusiwe uraisi uko kwa kabila moja mfululizo. Raisi ana mamlaka makubwa juu ya watu wake ni lazima awe ni mu ana hekima kisha si mgonjwa awe ni mtu ana afya yake hana ugonjwa wowote mbaya. Awe pia ana bibi, hawezi kuwa raisi yeye mwenyewe ikiwa hajui watu wake atawachukua vipi, ataishi vipi na familia hajui, yeye akiwa raisi ni bachelor atawezaje kumuhudumia mwananchi wa kawaida na hajui shida ilioko nyumbani. Atajua ya mtu mwingine alioko kado ikiwa shida ya nyumbani kwake hataiweza ataweza kumuhudumia Mkenya alioko mbali hamjui kabisa hata hamjui jina, hajamuona hata siku moja. Kwa hivyo yunaomba Katiba hii isiwakubali wa raisi ati kwamba yeye akae ni bachelor. Umesikia kwenye magazeti kwamba hata huko Amerika wale Mapadiri na ma Pope wanawashika watoto wakiwafanya vibaya. Je kutakuwa kuna maana hapo, raisi akipatikana na kashifa ya aina yoyote hafai kuwa raisi na hii nataka itiwe kwenye Katiba. Akipatikana raisi amefanya kashfa ya aina yoyote Wananchi wamtote kwa maandamano. Hatutaki kungojea atolewe na Commissioner wala na wabunge Wananchi wamtote kwa maandamano, ipitishwe kwenye Katiba. Itengeneze Katiba nzuri itakayotufaa wa Kenya tutengeneze Katiba ya kuwafaa jamii moja wala watu wa kabla fulani peke yake. Twataka Katiba ya kutufaa sote wa Kenya. Naona mimi hayo ya metosha mengine tutawapatia ma Commissioner. Asanteni.

Com Salome: Karibu tena kwenye kikao chetu cha alasiri na wa kwanza kutuzungumzia alasiri hii atakuwa Mohammed Ali

waziri. Hajafika bado, basi nitamuita Hassan Abdalla. Pia hayupo. Basi tutampata Mohammed Namad.

Mohammed Naman Mohammed: Honourable Commissioners, respected elders in this community ladies and gentlemen my names are Mohammed Naman Mohammed. I am a resident of Bondeni. My views on the Constitutional review of Kenya Commission are as follows. We should have a president who should be above politics and tribalism. That he should be a national figure. Also the president must have his running mate while contesting for the seat. We should also have a prime minister who will be in charge of the parliament and also running of the government affairs and also he is questionable to the parliament and the government. The deputy prime minister, which take charge in absence of the prime minister. The prime minister and his deputy as presently in Kenya like the speaker and the deputy speaker the parliament should elect a prime minister and his deputy just the same way as we are electing the speaker and his deputy.

Introduction of chief minister in the provinces; there should be Chief Ministers appointed in the respective provinces or we might call them regions and also the MP for those regions they should have an assembly of the region and it should be headed by the Chief Minister of that region and they will sit on quarterly system that is every after three months. They will have no salary as they are ministers of the government, sorry they are elected MP in the central government so they will not be paid in the region. The salaries will be from the central government.

The president will elect the ministers, assistant ministers, head of civil service, CGS, Service Commander and also the parastatals heads. The council should be given more powers and monopoly so that they can run the affairs smoothly and also they must get the cut at least 20% from the income of the parastatals in those regions so that they can take charge of the head facilities in the municipals, roads and also education. As a Muslim the Kadhis or the Chief Kadhi should be given more powers and jurisdiction be expanded.

In human rights they should be an Act of Human Rights such as the brutality of the police force. They should be thought how to handle the public. Also the use of fire arms of the extreme force by the police force should be reduced.

Regarding citizenship, naturalization of citizen should not be allowed to hold high offices such as parliament or the presidency as in the present Act it is that some ministers in charge of citizenship can revoke anytime the citizenship. So if we allow naturalization of citizen to hold higher offices such as parliamentarians or president then we can wake up to see that one-day our president citizenship has been deciphered.

Also in human rights we should see that in health facilities the reasonable bills in hospital and also over crowding of patients in hospitals. And also the patients must know their rights in hospital as one day a certain fellow of mine went to the hospital with his wife and he was forced that the wife should be operated because she wanted to give a birth. After refusing she was chased away but by sheer luck his wife gave birth without operation so the patients must have their rights in hospitals. And also the

patient with this cause or infected with HIV should be given or must be given the drugs free of charge and that is all I thank you so much for giving me this opportunity.

Com Salome: Asante sana Bwana Mohammed. Kuna swali kwa bwana Mohammed.

Com Wambua: Let me address you in the language you spoke. You said that there should be prime ministers in the regions rather than in the provinces but you did not tell us how the chief ministers should be appointed or elected and what could be their functions so can you elaborate that. That is number one, number two is that you said that chiefs should have more powers and the jurisdiction extended, powers to do what, to be the president or to do what. If you must be specific let us have a specific proposals regarding specific issues. When you say power to give the Kadhi or power to do what, power to rule or power to appoint ministers so can we be more specific on the powers you want to be restored on the chief Kadhi. And then lastly I think you mentioned something to do with MPs in the regions being based in the central government. Looking at the pattern which you have suggested you seem like you want the regions to be independent in a way but yet you are saying the MPs in the regions should be paid salaries from the central government. So what is emerging is that we have cut the devolution of power, what structure, will clarify on the structure that you are talking about?

Mohammed Naman Mohammed: I have said regarding the ministers. The ministers will be appointed by the president and it is the same ministers who will be called chief ministers in their regions. This has been done in Botswana, I have stayed in Botswana for five years so I have seen this things practiced there.

The power of the Chief Kadhi, the Chief Kadhi now discuss marriages and divorce and inheritance so they should be given more accessible into criminal laws in wife beating in the Islamic. In wife beating all domestic affairs, they cant deal with violence for example if the husband is violent to the wife the only solution presently the chief Kadhi or the Kadhi can do is just to separate them.

Com Pastor Ayonga: You talked about the hospitals of congestion and the patients rights but I didn't get you say in order to eradicate this congestion there should be this and that to cater for that congestion and for the patients rights you didn't elaborate this rights, that right.

Mohammed Naman Mohammed: In my opinion is that an Act should be formed so that the patients can get their rights. So it is the professionals who can sit down and look into this matter.

Com Salome: Asante sana Bwana Mohammed. Sasa tumpate Miano Kihu.

Miano Kihu: My name is Miano Kihu I am hear on behave of members of the Common Wealth Association Kenya Chapter.

Our presentation is only matters to do with press freedom and to some extent freedom of expression. Ours is a Memorandum. To begin with as an introduction you will not that in our current Constitution we do not have any provision for press freedom because you will find that press freedom is not engaged in the Constitution. Despite the big role that the press play in development and democratization process, in Kenya we seem not to have or our government seem not to have appreciated it's contributions. The result is that the government usually refuse press particularly the independent media with a lot of suspicions rather than a partner in development. In order to really institutionalize the make in Kenya as an important pillar of democracy we have the following 13 points recommendation to make. First we are urging this honourable Commission to include a clause on press freedom in the new Constitution.

It is our suggestion that such a clause should be expressed enough to guarantee Kenyan satellite. Section 79 of the Constitution on freedom of expression as it is today does not properly cater for the freedom of expression. This particular section, that is section 29 talks about guaranteeing Kenyans their freedom of expression, it has very many negation and also it is subjected to very many other level scriptures which make the work of journalist communicators and the Kenya's public to be very difficult. Such Acts are the intercession of Public Security Act, National Security Act, Official Secret Act, Defamation Act, Impression of Privacy Act, Books and Newspapers Act, Public Order Act, Themes and Stage plays Act, Armed Forces Act among others. This literally leaves no guarantee for the enjoyment of freedom of expression or the press for most of them are exercised in a bacillary manner.

Our second point is on prior arresting and censorship. We have seen that in the world today press censorship has been described as the first instrument that is governing the government, which are deviating from the democratic ideal use. Therefore we are urging this Commission to abolish all forms of prior arresting and censorship that is unjustifiable speculated and implemented in a bacillary manner. You will find that currently as the law is the government officer who are empowered to censor the press or sealing for that matter they enjoy a lot of leeway and the powers of this officers are often exercised in a bacillary manner. More so we have found many cases of publication being banned, others impounded and at times even in session of different places have occurred whereby the different places there are disabled.

The provision of these officers to burn disabled printing places and to impound publication should be clearly provided for in law and should be derived in a judicial manner. In order to protect Kenyan freedom of information and the press we feel that the media arresting or censorship should meet the following three conditions.

First they must be prescribed by law and never applied at bacillary, as it is common toy.

Secondly we want such prior arresting and censorship to be legitimate and proportional to the aims being pursued. This is to avoid a situation whereby there is witch hunting or economic sabotage of a certain publishing firm which are regarded as being un establishment.

The third condition they must be demostably necessary in a democratic society. We are really concerned with the recent bill

which are pending for tabling in parliament prepared by the Attorney General and we feel this bill goes contrarily to the spirit of press freedom and democracy.

Our third point of the memorandum we are seeking shield laws for journalism. It is our suggestion..... interjection.

Thank you very much. So we are also seeking shield law for journalist. This is where by journalist should not be forced to disclose the source of information where information concerned is on public measure. We are also suggesting to this Commission to ensure that the current principle where by the government is totally protected against public scrutiny to be contacted so that the public rights scrutiny to the government is ensured. For this matter since the peripheral of information includes laws from government institution, we are suggesting that from now hence forth, the institution which are publicly funded including the parastatals must be obliged by the Constitution to publish their books of accounts.

Our fifth recommendation is protection of three seats even seats in error. Here we have to pin point the current statute on incitement, charges of incitement or publishing alarming statement etc. so we feel those against the sprit of this stage.

To go quickly over the points we are also suggesting for this Commission to provide for development of community Radio stations. As the situation currently is you will find that there are many communities which are living in the periphery of this country and they virtually lack any access to the media which happens to be concentrated in major towns. the example is like the Elmolos who live in Turkana, Bajunis, Maasais, Ediroi Communities, Dorobos etc. so we are suggesting that this Commission it sees the need of putting in place laws that will support development of radio stations.

We are also, on our other point is that we want the laws to allow live coverage of parliamentary proceedings.

Another point, we are thinking that the public funded Kenya Broadcasting Corporation is to be manned by a board which has been approved by the parliament. the directors in such boards should be professional people and people who are independent and able to ensure balance and meet public expectation of that corporation.

We are also thinking that the Communication Commission of Kenya be also independent.

Last but not least we seek this Commission to recommend consolidation of the Media Law, all the laws created to the media. Currently we have CASA Statutes which are about 17 different Statutes, we do not have a consolidated and harmonized media law to deal with the press and we would like also our Commission to recommend existence of self regulated media in this country. Thank you very much.

Com Wambua: (inaudible).

Miano Kihu: We prepared it as a chapter, Kenya Chapter.

Com Salome: Sasa ningetaka kumuita Getrude Mwalake,

Getrude Mwalake: Kwa jina ninaitwa Getrude Mwalake. Nashukuru sana kupata hii nafasi na kuja kusema kwa niaba yangu na majirani zangu mtaani. Langu ni hili, ningeomba hii Katiba ifundishwe kuanzia shuleni. Igawanywe kwa watoto kulingana na umri wao. Hii itatusaidia kuwa mtoto akisoma shuleni atajua haki zake mapema kwa sababu unaona kama sasa mtu kama mimi nimekaa hapa sijui Katiba ikoje, sijui ile cover yake ni red ama ni blue. Ikisha tengenezwa hii Katiba ipelekwe ma- bookshops watoto wafundishwe, group za kina mama wapewe ipelekwe mpaka makanisani na pahali watu wanapokutana. Isiwe ya siri ya kukutana kotini peke yake. Kwa hivyo hapa nazungumza sina hakika yoyote ama ni Katiba ama nini kwa sababu hatujawai kuona Katiba.

Ningependa kama mwanamke akiolewa na bwana ambaye si wa nchi hii yule bwana na wale watoto wafanywe wawe katika nchi hii. Kwa mfano mimi ninaolewa na bwana wa Kitanzania na mimi nimeishi hapa Kenya nimezaliwa hapa. Unasikia kuwa yule bwana si Mkenya ama wale watoto hawatasajiliwa kama wa Kenya. Kwa hivyo ningeomba kama vile ndugu zetu wavulana wakioa msichana wa Kizungu ama huyo msichana wa Kitanzania yule bibi anaambiwa yeye ni Mkenya. Lakini yule bwana yake, kama mimi bwana yangu hatadhaminiwa. Ningependekeza wa Bunge na ma-councilor na raisi awe na miaka ya uzeeni, ya ku-retire. Asiende mpaka miaka sabini, miaka sitini. Miaka iwe hamsini na tano, akitaka kugombania u-councilor ama u-bunge ama raisi aanzie miaka thelathini na tano mpaka hamsini na tano. Na hii miaka mitano ya kuwa Bunge ama kuwa councilor Tumeona kwetu haitufai., ningependelea miaka mitatu imetoshwa, amefanya Maendeleo hakufanya atolewe.

Tungependelea mama, hii ni kwa niaba ya kina mama sisi wa Kristo. Mama akifiwa na bwana yake.....(interjection) mama akifiwa na bwana yake basi uridhi husumbua, watu wa bwana hujitokeza na kusema wewe hukuwa bibi halali na Kisheria kwa Islamu hiyo hakuna lakini sisi wa Kristu tunapata taabu tukiambiwa hukuolewa kanisani. Na shida ya kutoolewa kanisani ni kutokana na wazazi wetu. Mzazi anadai mahari kama laki moja ambayo yule bwana hana na sasa nimekaa na huyo bwana kwa mfano nina watoto wa tano ama watoto wanne na amekufa. Hiyo mahari ya laki moja hakupewa sasa hapo fujo huanza mahari iende kwa watu wa bwana na mimi hubakishwa na watoto nikipata taabu. Mwisho hao watoto ndio wanachangia group ya chokora.

Sasa ningeomba mtuwekee miaka ya kukaa na mwanamme hata kama hajatoa chochote kwenu at least miaka sababa miaka kumi imekaa na huyo mtu ni kuonyesha nyinyi mlikuwa ni bibi na bwana. Ni uwezo tu hakuwa nao wa kukuoa.

Mali ya umma; tungependelea mali ya umma isiuzwe na serikali kwa sababu siku zijazo ningependelea kujengwe kitu kama university hapa Mombassa, kujengwe kama polytechnic kubwa kubwa lakini hadi sasa Tumeona mali imeuzwa, hatujui watoto wetu siku zijazo wataenda university Nairobi na sisi wengine hatujui vile tutawapeleka huko Nairobi kwa hizo universities. Kwa hivyo tungependelea ya serikali iangalie ile mali ya umma iliyo chukuliwa na Wananchi binafsi, inawatajirisha wao sisi tunapata taabu.

Chokora; hawa ni watoto majority ukiangalia ma chokora ni watoto wa Kikristo na hii ni kwa sababu Sheria ya kuwa msichana akipata mimba yule mtu aliyempatia yule msichana mimba alazimishwi ama Sheria haiko ya kusema ni lazima amuo. Kama kwa mfano msichan yule form two na amepata mimba na kijana wa form three, kwa nini wale wazazi wasipewe jukumu ya kukaa na yule mtoto kwa sababu kesho tutamtupa, atakuwa chokora. Nimemaliza.

Com Salome: (Inaudible)

Getrude Mwalake: Ni kama nilivyosema hapo mbeleni, Katiba hatujui na hatujaiona, shida inatokea pahali tunaenda tunashitakiana na huyo kijana mwisho unaambiwa hakuna pahali alikuoa kwa hivyo rudi. Sasa unashindwa angekuoa wapi na mahari ni kama hiyo uliambiwa laki moja na kijana mwenyewe hana hiyo laki moja.

Mali ya umma kama ni vile inakuwa ni lazima iuzwe basi ama isiuzwe, tuna wasi wasi ikiendelea kuuzwa kesho tutajenga waopi kama kitu kama stadium ijayo ama university. Sasa tunaomba serikali izuie na sijui ina shida gani kubwa kuwa mpaka hiyo mali inauzwa.

Speaker: (inaudible)

Getrude Mwalake : Kusema ukweli hatujui mali ya serikali wala majumba ya serikali. Kitu kinatufanya tunajua hiyo ni mwangaza kuwa labda ile chifu anakaa tunasikia ndio ya serikali. Kwa hivyo tunajua ni mali yetu kama watu wa nchi hapa. Na ardhi ni kama hivyo tunasikia pahali ile plot ilikuwa ilikuwa supposed iwe ya serikali.

Com Salome: Asante sana mama Getrude. Njoo pale ujiandikishe. Sasa tumpate mzungumzaji mwingine.

Abdullah Salim: Jina langu kaili ni Abdulla Salim. Salama maleku. Ninazungumzia kuhusu mambo ya shirigazi ya Kadhi, ndugu nzetu walifika walitangulia. Kuhusu chifu Kadhi na Kadhi mkuu tunataka awe na degree mbili. Awe na elimu ya Kiislamu na awe na elimu ya Kiingereza anaweza kusimamia koti zote.

Ya pili naomba serikali iweke committee ya kuchunguza kesi zile wakihukumu. Ya tatu naomba serikali kupiga marufuku vipindi ambavyo hazifai kuonyeshwa watoto wetu mazingara ya nje, si mazingara ya hapa kwetu. Kama hizi vipindi tunaonyeshwa katika matelevishoni zetu za KTN, KBC na hizi ma kampuni za binafsi. Inapoteza watoto na kuharibu kwa watoto wanakuwa hawana tabia njema na wazazi wao kwa sababu sisi wa Kenya kila Mkenya ana mila yake na desturi yake ya kiheshima. Mkubwa ana mheshimu mdogo na mdogo anamuheshimu mkubwa. Sisi Waislamu tuliambiwa na Mtumwa wetu.....msipandishe sauti juu ya mkubwa wako. Awe mke awe mme, wewe umezaliwa mkubwa wangu wa kike sina haki kutoa sauti kubwa kwa sababu ni mme, la, lazima uwaheshimu ndio desturi za kimila za kikwetu hapa Waislamu na mila

ingine ya Kikenya kila mmoja anajua mila zake na heshima zake na desturi yake.

Ya tatu, naomba serikali itiliwe mkazo Sheria yetu hizi za Koran tukufu ambaye ndio urasi wetu na kila kitu yetu iko katika kitabu chetu, Katiba hiyo ya mwenyezi Mungu hakuna Katiba ingine, sisi tunaamini hiyo salama maleku . sina maneno ingine, mwenye swali aulize.

Com Wambua: Umesema Chief Kadhi awe na degree mbili moja iwe ni ya Kiislamu ingine ya Kizungu. Degrees hizo ziwe za kisheria ama ziwe za dini maanake degree inaweza kuwa ni ya Sheria iwe ni ya Kizungu, iwe ni ya Kisheria.

Com Salome: Kama hauna jibu kwa sasa ni sawa maana ukipata hil jibu utatuandikia. Asante. Na sasa tupate Samuel Tsuma.

Samuel Tsuma : Nina shukurani sana bwana Commissioners wote mlio hapa nataka kutoa shukurani zangu ma- Commissioner wote mlio hapa, ma dungu wote, jina langu naitwa Samuel Jembe Tsuma na ni mmoja wao katika wazee waliohapa mjini na nimeonelea ya kwamba na mimi pia nitoe maoni yangu juu ya Constitution ya Kenya ambayo inatungwa.

Katika maoni yangu ni ya kwamba tungekuwa na originalism, yaan serikali ya majimbo kama vile wanavyo fanaya United States of America. Kila jimbo na governor wake na mambo yao lakini wana president mmoja ambaye huyu uchaguliwa na majimbo yote. Na vile vile hapa Kenya tungekuwa na president mmoja na majimbo yakawa ni yale manane ambayo majimbo haya yangukuwa na deputy president, yaani president wadogo ambao katika jimbo lile wangepikiria mambo yao ya kimaendeleo. Kwa mfano hivi sasa hapa Coast hakuna hata university moja, sisi kama Wananchi wengine lakini kila ile keki kubwa ikija hatujui inaenda wapi kwa hivyo sisi tunasalia kama third class citizens na hii inaudhi sana roho. Na hawa mawaziri ambao wangukuwa ma deputy president ambao wangukuwa katika majimbo pia vile vile wangepikiligwa kila baada ya miaka tano ikiwa wamefanya vizuri, ikiwa wamefanya vibaya basi wakati wake utakuwa huo huo maanake tutakuwa tushaona mazuri yake na mabaya yake.

Na katika majimbo haya yangukusanya mapato yao, mapato yao ingewawezesha kujenga hospitali nzuri, wakanjenga ma – universities ma nzuri ili watoto wetu wakatalii vizuri kwa kila section, wakawa kama wenzi wao katika dunia. Kwa hivyo hii ingewaletea watoto wetu pia madaraka ya kuandikwa kazi kutegemea qualifications zao. Si mtu kuchaguliwa tu kwa sababu yeye ni familia ya ABC, hiyo nisingelitumika kabisa.

Jambo lingine ni hawa madungu zetu ma chief wanachaguliwa na serikali. Utakuwa uko mahali uone mtu huyu ambaye ndio alikuwa humjui, hajui desturi zenu, hajui vile mnavyoishi, hata kile umuambialo yeye analiona kama ni upuzi, unachukuliwa kama kinyagu maanake. Kwa hivyo mambo kama hayo yangelikuwako, ma-chifu wangepikuliwa na Wananchi wenyewe kwa sababu Wananchi ndio wanawajua desturi zao, wengine pengine huwa ni walevi, wana tabia mbaya lakini ikiwa wamepita interview huko basi utamuona yualetwa hapo tu na kirauni eti ni chifu wako. Hayo nafikiri yangekoma.

Jambo lingine ni habari ya industries; tulikuwa na industry yetu hapa ya miwa hapa Ganzi pia tukawa tuna ile Dixco factory na Cashew nuts huko kilifi, hizi zote ziliuwawa makusudi ili watu waendeshe kiviao kwao, je sisi tutamwendea nani? Ikiwa twakamuliwa tu hatuna chochote tunachotaka, watu wetu wanaangaika kwa uhumi, uchumi umekuwa taabu kwa sababu hakuna factory yoyote ya kuweza kuwapatia riziki, kwa hivyo haya ndiyo yanaleta uchungu katika roho zetu ili kwamba serikali ikiwezekana ifikirie sana habari hii.

Pia ningeliomba tupatiwe national schools, walete waalimu wazuri namtu akipita hapo aende chuo kikuu mara moja, kwa hivyo sasa hatuna hata kimoja. Basi kwa hivyo sasa Tumetegemea kuomba omba kama mayatima. Je hali hii itaendelea nayo mpaka lini? Naomba ikiwezekana ifikiriwe sana jambo hili, lizingatiwe ili kwamba na sisi tujuie kama tuna mwelekeo fulani.

Hata pia kuna vile viti vya specialty elected members of parliament, huku Coast naona mambo tu yanapita hivi hivi, wako watu ambao wanatosha kabisa kukauliwa, watu wanaojua desturi za watu mashaka yao, lakini hawapewi hata nafasi moja. Kwa hivyo tunaomba ikiwezekana pia hili pia lifikiriwe.

La mwisho kabisa, tungekuwa na educational committee hapa Kenya Republic ambayo inge-oversee ile standard ya elimu na pia wale waalimu wanaofanya bidii katika skuli zao wakipitisha watoto wangepata nafasi ya promotion ili kwamba nao vile vile wakapata matund/a ya uhuru. Ni hayo tu, asante sana ma Commissioner na ndungu zangu wote.

Com Pastor Ayonga: Bwana Tsuma, umesema majimbo, tuwe na majimbo namna ile ya United States of America ambayo yanaongozwa na president na kila jimbo kuwa na president mdogo. Nadhani Amerika kila jimbo linakuwa na governor, halina president, president ni mmoja lakini katika majimbo kuna ma- governor. Je ulitaka kusema ma-governor au wewe umetaka katika maombi yako kwamba kiloa jimbo liwe na kiongozi anayeitwa peresident.

Samuel Tsuma: Tuseme katika maoni yangu kwa sasa angekuwa vice president ili wampe mawaidha au advise yule president Head of State. Baada ya akiwaona wenyewe kwamba(interjection) exactly, ndio hivyo tu.

Com Salome: Asante sana bwana Tsuma. Sasa ningetaka kuipa hii nafasi kwa Abdilai Mwinyi.

Abdilai Mwinyi: Kwa majina ninaitwa Abdilai Badi Mwinyi, chairman wa Majengo Umoja Youth. Ningependa kutoa mapendekezo yafuatayo ili kuwa na nafasi nzuri za uongozi katika serikali inayokuja tunataka Katiba ambayo utawala ya mikoa hasa ma chifu na manibu wao, ma DC na ma DO, na ma PC wote wachaguliwe na wanainchi. Wachaguliwe wapeleke vutambulisho viao vya kutibitisha kwamba wao wana ujuzi wa kufanya hiyo kazi kwa Tume ya uchaguzi halafu nafasi hizo zitangazwe kuwa wazi na kufuate utaratibu unaofuata hapo kwamba siku ya kwamba kufanywe uchaguzi ambao raia na wazee wa mitaa watachagua ma- assistant chiefs. Siku ya pili ma- sub-chiefs wataokuwa wamechaguliwa wachague ma-chief kupitia

delegate system. Halafu siku ya tatu ma – chief wataokuwa wamechaguliwa wachague ma DO. Siku ya nne ma DO wataokuwa wamechaguliwa wachague ma DC na siku ya tano ma DC wataokuwa wamechaguliwa wachague ma PC na wote watakao chaguliwa wawe ni waakazi wa eneo wanaofanyia kazi.

Mvumo wa kiserikali uwe mvumo wa majimbo na kuwe ku;mechaguliwa ma –governor ambao ndio wataokuwa wakuu wa majimbo na wawe pia ma governor hao ni wazaliwa wa maeneo hayo wanaotoka.

Kuwe na uhuru wa dini, mtu asibaguliwe katika kupewa huduma za kiserikali eti kwa sababu anatoka dini fulani. Hatua kali ichukuliwe mtu yoyote anaye toa huduma kibaghuzi.

Swala la ardhi; ili kupunguza tatizo la masquatter mtu yoyote anayetaka kununua ardhi na ardhi hiyo ina mtu anaishi hapo ndani ama kuna miti yake. Board inayotoa mashamba isikubali kumpatia huyo mmnunuzi ardhi mpaka kwanza aelewane na yule anaye kaa katika ardhi hiyo. Anapokubali ule anayekaa katika ardhi hiyo basi awe atauziwa na yule anayekaa katika ardhi ile ama kuna rasilimali zake hapo akikataa asilazimishwe.

Kuwe na utaratibu mzuri kuhusu huduma ya polisi. Polisi asikamate mtu yeyote pasi na warati. Pasi ina kujitambulisha kwa kutoa kitambulisho chake na awe amevaa uniform maalum za polisi na uniform hizo ziwe zinaonyesha wasiwasi nambari zake za polisi. Hii itaepusha tabia ambayo iko hivi sasa ya watu wanaoweza kuvamia watu na wakasingizia hao ni polisi wakachukua watu badala ya kuwapeleka kituo cha polisi wakaenda wakawapeleka pahali pasipojulikana wakawapoteza. Kwa hivyo tunataka polisi kwanza ajitambulishe yeye ni nani na atoe kitambulisho chake cha polisi na awe anatambulika kwa sababu amevaa uniform, nambari zake za polisi ziko wasi wasi zinabainika kwamba ni polisi fulani amekuja na nambari zake ni kadhaa.

Kuwe na taasisi maalum ya kutetea Wananchi wanyonge wasiokuwa na uwezo wa kutia mawakili hasa pale wanaposhikwa nyumbani kwao wamekaa ama usiku mtu akitoka kazini anashikwa na polisi halafu anazingiziwa kuwa amekamatwa akiwa mlevi na. Kukosa adabu. Iwekwe tahasisi maalum ya serikali iweze kutetea watu kama hawa.

Sheria yoyote ambayo itapitishwa na Bunge na ipate asilimia sitini na tano ya kura za wa Bunge, basi raisi hana budi lazima atie sahihi, hana hiari.

Councillor, Mbunge na Raisi aisyewatumikia watu wake ipasavyo Wananchi wawe na uwezo wa kumfuta kazi. watamfuta kwa kukusanya thuluthi moja ya idadi ya kura alizopata halafu apelike sahihi hizo kwa Tume ya uchaguzi halafu Tume hiyo itangaze kuwa nafasi hizo ni wazi na Wananchi wawe uhuru kuzipigania.

Serikali itilie mkazo maswala ya walemavu. Kila Kampuni na mashirika yote ya kiserikali yahakikishe asilimia kumi ya wafanyi kazi wake wamechukua wasiojiwezi, yaani walemavu. Kutengwe asilimia fulani ya mapato ya serikali kuwapa allowance kila

mwezi walemavu. Wananchi ambao hawana kazi wapewe allowance ya kuwasaidia maishani. Serikali ifutilie mbali usajili wa ardhi zote zilizoporwa na waporaji.

Swala la uraisi; raisi awe chini ya Sheria na asiwe juu ya Sheria. Uwezo wa kuvunja Bunge uwe wa Speaker, uwe ni uwezo wa Speaker wa Bunge. Muhula wa Bunge unapomalizika Speaker avunje Bunge kuwe na serikali ya mpito mpaka serikali nyingine itakapochaguliwa. Serikali ya Mpito itoe mamlaka kwa raisi mpya muda wa wiki mbili baada ya kuchaguliwa raisi wetu.

Mbunge awachuwe kazi yake ya kuwakilisha watu waliomchagua na asipewe kazi nyingine kama za waziri na kadhalika. Hiyo itasaidia wa Bunge kuwakilisha watu wao ipasavyo badala ya kuchaguliwa kwa waziri na aende akakae Bungeni awe ni mtu wa kunyamaza tu watu wake wanateseka huko. Kwa hivyo awe ni Mbunge anawakilisha watu wake.

Kazi ya waziri zipewe mtu yoyote ambaye elimu yake ni ya juu na zigawanywe mikoani kote pasipo na ubaguzi. Ma-bar yasiyengwe katika nchi mji na iwe mbali na sehemu za Ibadha kama vile msikiti na makanisa. Iwe ni hatia mtu kufungua bar katikati ya mji.

Uhuru wa kuabudu ni kwamba serikali itilie mkazo swala hilo na kuhakikisha uhuru huo kila mtu aukumiwe kulingana na Sheria za dini yake, awe Muislamu ama Mkristo. Asante.

Com Salome: Asante sana Abdilai. Kuna maswali?

Com Pastor Ayonga: Bwana Mwinyi.....(inaudible)

Com Wambua :(inaudible)

Abdilai Mwinyi: Kujibu kwangu ni kwamba kama tunavyojua swala la uongozi ni swala ambalo hilo lazima serikali ishugulikie sana. Hatuwezi kusema kama kuna uongozi mbaya katika vijiji ama katika ma-location na ma wilaya halafu serikali ishindwe njisi yataweka kiongozi kupitia njia gani. Ikiwa Wananchi wanalalamika kwamba hatutaki kuweka kiongozi ambayo hatumjui anatoka wapi, hajui shida zetu halafu badala kutatua tatizo hilo serikali iseme hatuna pesa kushugulikia shida yenu, hapo itakuwa iwezekani. Ni lazima ijulikane njia fulani itapatikana hata kama delegate system itachukua siku moja au mbili lakini matakwa ya Wananchi ni kwamba serikali iwe wale viongozi ambao watachaguliwa wawe ni watu ambao wanatoka maeneo yale wanatoka na hiyo delegate system tunaiona imefaulu si kwamba kwa sababu ya hii tu ni mpya imekuja, vyama vingi vya kisiasa vimetumia hiyo njama na ninafikiri ndio njia moja ambayo inagarimu pesa kidogo kuliko system zote.

Kuhusu swala la wadhifa; ni kwamba wale wataochaguliwa wote ni wale ambao watakuwa wana ujuzi wa kufanya ile kazi na

ndio maana itatangazwa nafasi za assistant chief, nafasi za ma DO zitatangazwa na vyeo mbali mbali. Sasa wale ambo wako interested kwanza kabla hawajarudisha kwa Wananchi kuchaguliwa wao wamepeleka form zao za maombi na qualification zao. Wakipitishwa huko na board ianhusikan na ma swala hayo sasa ndio watarudisha kwa Wananchi. Ikiwa ni mmoja hana mpizani tutasema hana mpizani, lakini ikiwa ana mpizani wata challenge huko mashidani. Lazima achaguliwe kupitia hizo kura.

Com Salome: Asante sana Bwana Mwinyi. Janet Wamahiga yuko? Haya sakafu ni yako.

Janet Wamahiga: Kwanza ningetaka kurudisha shukurani sana kwa Commissioner kuletwa hapa kwetu ili waweze kusikia mambo yetu na Wananchi wenzangu Hamjambo. Mimi ninaitwa Janet Wamahiga Mirobi, mimi ni chairlady wa KANU katika Thaironi Ward na nina wakilisha ggroup yangu ya Thaironi Women Group. Ya kwanza ningetaka kwamba kila yule anayetaka kusimamia uraisi atangaze utajiri wake. Pia awe na umri unaozidi miaka hamsini na kuendelea mbele. Madiwani nao wawe wamehitimu mpaka kidatu cha form four.

Ya pili wanawake wapewe madaka katika Bunge na pia katika ma ofisi za serikali. Ya tatu tunataka wanawake wapewe haki kama wanaumme kwa mfano Mzungu akioa msichana wa Kenya akifika huko anapewa uraia wa huko. Mimi nikiolewa hapo na Mzungu akija hapa ni shida awezi kupata uraia wa Kenya.

Mapolisi wetu wasiwe wakifutwa kazi na kama amepewa retire ajulikane ako mahali gani sababu uhalifu mwingi umepatikana kutokana na hawa waliowachizwa kazi.

Engine, wazazi lazima wapeleke watoto wao shule, watoto wapewe haki zao. Pia mtu yoyote atakaye patikana na mtoto chini ya umri wa miaka kumi na nane apelekwe kotini na kuhathibiwa vikali.

Kuhusu passport za Kenya imekuwa ni vigumu sana kwa mwananchi kupata passport ama ID ni shida sana kwa mwananchi wa Kenya kupata hizo vitu. Lazima mambo haya yaangaliwe vilivyo kutatua hizi shida za ma passport na ID.

Speaker: Asante Bi Chair. Mimi swali langu ni kuhusu nafasi za kazi za Mbunge. Msemaji amesema wa kina mama wapatiwe nafasi za Bunge sawa. Sasa sijui kama ni zile kazi kama za ukarani ama wa Bunge wawe sawa wake kwa waumme kwa sababu kama ni kazi za Ubunge basi ni raia mwenyewe mwenye kuchagua na kama ni ziwe sawa sasa sijui anataka iwe sawa ama wanachi waambiwe lazima wachague mwanamke ama iwe vipi. Pengine angetueleza zaidi ya hapo.

Janet Wamahiga: Kusema hivyo ni kwa sababu kuna viti ambazo huwa zimetengwa kwa nominated MPs kwa hivyo wakati zinatengwa pia wanawake wapewe.

Com Salome: (inaudible)

Evans Gachie: Hamjambo Nyote? Mimi ninaitwa Evans Gachie kutoka kwa shirika la Young Leaders Network, vijana viongozi, mtadawazi wa vijana viongozi. Kwanza nitaanza kuzungumzia kuhusu vijana. Ni wazi kwamba vijana Tumetengwa sana tangu tupewe uhuru katika hii nchi ya Kenya sawa sawa tu na vile wanawake wamekuwa wakitengwa na Tumeona serikali zote mbili tangu zichaguliwe hazina sera maalum kwa mambo ya vijana hasa tangu 1982 Tumeona mambo mengi ambayo yamekuwa yakifanyika kugandamiza vijana katika serikali ilioko. Kwa hivyo sasa sisi kama viongozi vijana ndipo tunasema katika Katiba itakayokuja tungependa I-provide member of parliament for the youth halafu pia tungeomba pia tuwe na member of parliament for women kuwe na Bunge wa wanawake anawakilisha wanawake, yeye hana eneo anawakilisha tu wanawake na pia kuwe na Mbunge mwingine pia anawakilisha walemavu na makudi mengine yoyote ya wenye kasoro ndogo ndogo.

Pia kwenye hiyo Katiba tungeliomba katika hizi Commission uwa zinakuwa formed kuwe na Commission hususani iko pale tu maalum kushugulikia mambo ya vijana labda ingetafutwa jina lakini sisi tungependa labda iitwe National Youth Commission. Mnajua wazi kwamba toka mtoto akiwa mdogo anavyokuwa, uwezi kumfanyia mambo sawa na mtu mzima. Vile vile tunavyofanya mambo ya watoto pia vijana wafanyiwe mambo kiujana. Hii Commission ije na National Youth Policy kwa sababu tunajua tangu tupewe uhuru miaka thelathini na saba nafikiri Kenya hatuna sera ya vijana, National Youth Policy hakuna mpaka saa hii ninavyozungumza. Nchi majirani zipo lakini hapa hatuna sera ya vijana, aibu gani. Sasa hii sera labda itahusisha mambo kama reproductive health, tunajua ugonjwa wa ukimwi unahadhiri sana vijana, tunajua umasikini unahadhiri sana vijana, machokora ni vijana, mimba unapata watu wakiwa vijana ni kwa sababu hatuna hii sera, kwa hivyo hii sera iwe inashugulikia reproductive health, mambo ya uwajiri, employment, mambo ya kama education, education ambayo ita-allow vijana wapate civil rights information na pia hiyo sera iwe na mambo ya technological training na iwe na sera pia ambayo inayoshughulikia mambo ya mchezo kwenye hiyo policy. Nishamaliza mambo ya vijana.

Nikiingia kwa mambo ya serikali kuu executive, kuna serikali mara tatu. Serikali kuu executive tungelipenda sisi rais president awe ni ceremonial. Awe kazi yake ni kuhudhuria tu mikutano na kufungua na kukaribisha wageni, asiwe anaongoza serikali lakini awe tu anaongoza nchi. Kuwe na Prime Minister ambaye huyo ndio atakayoongoza serikali na pia raisi tungependa asiwe anawakilisha eneo lolote katika Bunge. Tungeliomba pia permanent secretaries wawe wakiwa appointed by the Public Service Commission on the basis of merit, expertise's, experience character and qualification. Tungependa pia secretary to the cabinet awe appointed by the head of government au Prime Minister.

Haya kuna ofisi moja mabyo Kenya hakina, Tumesikia watu wakizungumzia vile polisi wanatunyanyasa, Tumesikia watu wakizungumzia kuhusu vile viongozi wa serikali wanatunyanyasa. Je, hawa viongozi wakitunyanyasa huhwa tunaenda wapi, hatuna mahali pa kukimbilia lakini tungekuwa na ofisi of ombudsman hapo ndio tubaweza pahali pa kukimbilia, ofisi of ombudsman ni office ambao uwekwa kushitaki viongozi wa serikali, police na wengine wote ambao watatunyanyasa sisi katika serikali kwa hivyo tungelipenda Katiba itoe ofisi of ombudsman na ziwe ziko allocated from the divisional levels kwenda juu hata kwa location. Tungeliomba parliament iwe na uwezo katika Katiba ya ku-pass vote of no confidence to the government, na kukiwa na vote of no confidence basi hiyo serikali inatajikana i-resign immediately.

Tungeliomba pia hiyo Katiba katika upande wa local government, nafikiri hiyo ishasemwa, local government iwe elected sitaki kuregelea.

Halafu ningelipenda hizi Commission ambazo nitazitaja hapa ziwe zinakuwa approved by the parliament kabla hazijakuwa appointed. Ya kwanza ni Electoral Commission, ya pili ni Attorney General awe akipitishwa na parliament kwanza kabla hajakuwa appointed na zile Commission zingine ndogo ndogo za inquiry. Ingingine ni Permanent Services Boards and Hard Rock Boards zile ziko passed through the parliament. wengine ni executive chairmen, chairman wa ma-board of directors, executive directors, managing directors, general managers of the parastatals, wengine ni Public Prosecutors or any other prosecutor, wengine ni ma-Controller and Auditor General. Na hawa ma- Controller na Auditor General wawe wakituma report zao directly to the parliament na copy moja iTume to the treasury.

Halafu pia kuna ingine governance and the members of board of governance wa Central Bank of Kenya and the board of governance of any other public operation. Wawe wakipitia through the parliament kabla hawajakuwa appointed. However Judicial Service Commission of Inquiry should be exempted. Kwa sababu gani? Mtu wowote ambayo yuko kwenye Judicial Service Commissioner huwa ni Judge na Judge aki-appoint-wa lazima awe approved by the parliament kwa hivyo hawa Judicial Commission of Inquiry wanaweza kuwa exempted kwa sababu ma-judge already uwa washakuwa approved by the parliament. halafu kuna hii post ya Police Commissioner, we don't need a Police Commissioner in Kenya. All the Police Service and all the Police Department should be localized in home areas. Mapolisi wawe wana recruit-iwa kutoka kwa ile mitaa ambao watafanya kazi. Kama ni village ni town au ni municipal kama ya Mombasa polisi wana- recruit-iwa hapa kwa sababu wanajui ile eneo vizuri wanafanya kazi hapa hapa. Hatutaki polisi ambao atatolewa Nandi kuja kufanya kazi hapa kwa sababu kitu cha kwanza hajui lugha yetu, kitu cha pili hajui hata hii masikani za hapa vizuri. So inakuwa raisi kwa ma- asikari ku- recruit -iwa kwa zile maeneo ili waanze ku-detect crime kwa uraisi na pia wataweza ku-prevent crime kwa uraisi kwa sababu wao wenyewe ni wakaaji wa pale.

Ya mwisho nitaongea kuhusu mambo ya ardhi. Kuhusu land ownership; land ownership na ma-transfer za land should not be touched by the central government kama vile inavyoendelea saa hizi. It should be left to the state legislation and the local authorities. Ma-disputes, hizi muvurugano ya mashamba ziwe zinahusishwa na serikali yenyewe na Local Authorities na court of Law. Halafu president should not have powers on the land matters kwa sababu kwa saa hizi president ndio ana-appoint land Commissioner. Na. Kama president ana-appoint land Commissioner ni rahisi hata yeiye mwenyewe pia kuiba shamba na hatuwezi kumfanya chochote.

La mwisho kabisa ni kwamba all the public land, hii land yote ya serikali iwe inasimamiwa na land boards na court of law so that kukiwa na shida yoyote kama mambo ya land titles, boundary disputes and transfers ziwe zinafanywa na hizi boards na court of law na kuwe na mamlaka maalum ipatiwe kwa local authorities kama ni municipal waweze ku-deal na mambo ya land

huku chini. Hii yote itazuia masikini, tunakuwa masikini kwa sababu mambo yanafanywa na authority za huko juu na hizi local authorities huku chini hazina uwezo. Asanteni sana.

Com Pastor Ayonga: Kwa Polisi umesema kama hiyo force ingetolewa ni lipi lingewekwa kwa badala yake maoni yako ni lipi lingewekwa kwa badala yako kwa maana kazi ya polisi ni muhimu kwa vyovyote.

Com Salome: Hata mimi nina swali kwako(inaudible) kwani wanajua masikani kwa hayo na vile wataweza kuwakumbusha vilivyo wenye karibu Sheria(inaudible).

Evans Gachie : Asante sana. Swali la kwanza hatuitaji police Commissioners hapa Kenya kwa sababu police Commissioner kitu cha kwanza ana appoint-wa na raisi na mimi nimesema tungependa tuwe na polisi ambao watatoka mitaani ambao watafanya kazi kwa vile maeneo ambazo wanaelewa vizuri. Sasa mimi ninge-propose badala ya polisi Commissioner kwa sababu tutakuwa na hawa mapolisi watakuwa wame-recruit-wa mitaani kwanda juu police Commissioner iondolewe na instead tuwe na inspector general.

Halafu kwa swali la pili ni kweli kwamba saa nyingine tunafanya kazi katika maeneo sisi tunajulikana kuna mtoto wa shangazi, mtoto wa mjomba sasa kuna ile kwamba mtoto wa shangazi hatashikwa. Lakini tujue nafikiri hatufanyi kazi na mapendeleo. Otherwise tukiangalia hivyo ni kwamba hakuna mahali tutakuja fanya kazi. kitu ni kwamba kutakuwa na code of ethics na pia kuna professional code of ethics katika kila kazi na uwa kuna Sheria ina-deal na polisi, ninafikiri saa hii ni Chapter 84 of the Laws of Kenya. Kama hiyo Chapter inaweza ku-capture mambo ambayo yatamuwezesha polisi kufanya kazi kwa eneo la kwao basi hiyo chapter ya police Act irekebishwe pia kado na Katiba iweze ku handle huyu polisi ambaye anafanya kazi katika maeneo yao. Asante.

Com Wambua: (inaudible)

Evans Gachie : Asante sana. Nimezungumzia kuhusu Sheria ya polisi na nikasema kubadilisha jina hiyo ndio kitu ya kwanza kwa sababu kubadilisha jina itamaanisha kwamba pia majukumu yake pia yatabadilishwa kidogo. Tuseme police Commissioner basi ikibadilishwajina ni kwamba zile kazi police Commissioner alikuwa akifanya zita remain vile vile au zitaondolewa zote. Ni kwamba we are going to adopt, tutachukua vitu ambazo zitafaa na huu mfumo mpya halafu sisi wenyewe tutakuja na mfumo wetu vile tunavyopenda vijana wetu waandikwe kazi na vile ningependa tufanye nao kazi. kwa hivyo hii ni jambo ambalo mimi peke yangu hapa nilipo mimi singependa kuchangia peke yangu. Kwa hivyo wakati itawekwa kwenye Katiba basi sisi Wananchi tena tupewe nafasi ya kuchangia pia kwa ile Sheria ambayo ni ya police Act.

Com Salome: (inaudible).

Immanuel Gitau: Me I am Immanuel Kangethe. Ningeuliza swali moja, nawezaongea na lugha ya ki lugha yangu au niongee na lugha ya Kiswahili.

Com Salome: Unataka kuongea nna lugha gani?

Immanuel Gitau: Ninataka kuongea na kikuyu.

Com Salome: Okay, endelea na hiyo lugha maana kila mtu ana uhuru wa kuzungumza kwa lugha yoyote ile.

Immanuel Gitau: (*In Kikuyu*)

Translator: I am requesting that parliament should have a representative of disabled because if you look critically at the current parliament you find that there is no representative for disabled as per now. Kama nilivyosema ni kwamba kitu ya kwanza ningependa kuzungumzia kuhusu walemavu. Tukiangalia vizuri katika Bunge letu la hivi sasa ni kwamba hakuna walemavu ambao wanawakilisha walemavu katika Bunge. Kwa hivyo ningelipenda walemavu tuakilishwe Bungeni ili tuweze kuongea au kujadiliana kuhusu walemavu wenzetu.

Jambo la pili , ukiangalia katika huduma za kusafiri utakuta kwamba sisi walemavu huwa au katika vyoo vya umma sisi walemavu huwa hatushugulikiwi kwa kutolewa zile vifaa ambazo za weza kutusaidia sisi kuweza kushiriki katika hizi huduma za vyoo na usafiri wa umma. Kwa hivyo jambo kama hili lingeingaliwa ili sisi walemavu tuweze kushugulikiwa kikamilifu. Asanteni.

Com Salome: Asante sana Immanuel. Sasa ningetaka kumuita Omondi Kenneth.

Omondi Kenneth: Asante. Kwa jina ninaitwa Omondi Kenneth. Jambo la kwanza nataka kuchangia kuhusu walemavu. Ningependa Katiba iwekwe walemavu wasomeshwe kwa lazima

Omondi Kenneth: Jambo la kwanza nataka kuchangia kuhusu walemavu, ningependa katiba iwekwe walemavu wasomeshwe kwa lazima. Wapewe education, wapewe elimu ya kilazima mpaka ile ningependa education yao ifike form four.

Halafu kuhusu jambo la kikazi, wapewe uhuru wa kufanya kazi yoyote tu, sio eti walemavu wawachiwe tu washone viatu na nguo. Isitoshe wakitoka pale krudi huku pia wanapata kama serikali yenyewe wamemwaga mitumba nyingi, wewe ulifundishwa kushona viatu, hutashona viatu tena, ulifundishwa kushona viatu mpya, utakuja kupiga viraka. Sasa tunepende tutengewe kazi maalumu hasa tukitoka pale Cool Heart unakuja kupewa kazi.

Halafu jambo ingine ile ningependa kuongea ni juu ya mobility, zile viombo vya kutembea wasiwe wanaweka ile Kwa saa hii

ni ghali sana, kwa saa hii wanaonda kazi, sasa tungependa serikali watilie maanani maanake hizo vitu ni muhimu sana kwa walemavu.

Jambo lingine, katika haki ya walemavu, zamani tungekuwa tunapata zile free education na free training na wakati huu mlemavu kama mimi nikiwa nataka training mpaka nilipe pesa kiwango, hakuna institute yete ambaye mpaka ulipe. Sasa tungependa waweke tafisisi, serikali waweke tafisisi ambayo watakuwa wanachunguza ni kweli ile haki ambao walemavu wote wanasoma ama wengine wamewachwa kwa sababu tukisema walemavu wasome wengine watawachwa wengine watakuwa wanasoma.

Halafu tungependa sasa, kuna wazazi wengine wanatabia ya kuweka watoto walemavu dani ya nyumba wanaficha watoto wao, halafu shida ikitokea, akiwa mkubwa anamwacha nje. Sasa hakupewa education, hana kitu ya kufanya sasa inakuwa shida ikiwa ameshakuwa mkubwa. Sasa tungependa mzazi wowote ambaye yeye mtoto wake ni mlemavu anaweka ndani ya nyumba apelekwe kotini ajibu mashtaka gani kwa sababu anaweka huyo mtoto. Itakuwa wakati ambao mtu atakuwa mkubwa na ikiwa hajasoma atafanya nini?

halafu sasa jambo lingine pia ambao ningependa kuchangia ni katika kapuni nyingi haswa hakuna walemavu wanafanya kazi. Sasa tungependa kapuni ipewe kiwango fulani ya wafanyikazi walemavu. Na ni hayo tu ndio ningetoa.

Com Salome: Asante sana Bwana Omondi. Majina yako kamili ni nani?

Kenneth Omondi: Omondi Kenneth.

Com Salome: Asante sana bwana Kenneth. Sasa tumpate Paul Kitimbi.

Paul Kitimbi: Mimi ninaitwa Kitumbi Paul. Sasa points ambazo niko nazo ya kwanza ni sehemu ya basic rights. Hii ningependa wafanyi kazi wote wawe wana haki ya kuwakilishwa na trade union. Nikisema wafanyi kazi wote nina maanisha pia polisi, unitary forces, wako na problems ambao zinawahusu kikazi ambao wangukuwa na trade union wangeweza kusaidika kama wafanyi kazi wengine.

Nikija upande wa land property rights, ultimate ownership of land, should be an individual, not community, government ama tribe maanake ardhi uwa ni mali na hatuwezi kupima mali ya tribe ama community, tunapima mali ya binadamu mtu mmoja tu. Kusiwe na kipimo cha ardhi; hiyo ina maanisha there should be no sealing on land ownership.

None citizens should not own land.

A Kenyan citizen has a right to own land anywhere within the Kenyan boundaries. Government should encourage this by

resettling landless people irrespective of their origin to different areas of the republic kuliko kama mimi ni Mbaluyia ninawe resettled Ubaluyani. Iwe sehemu yoyote ambayo government ina-allocate land, inakusanya wale watu ambao hawana ardhi iwe ni Kisumu, Somali, wawe resettled in those areas. Hiyo ita encourage watu waelewe ya kuwa nchi haina mupaka.

I then go to cultural ethics and regional diversity; the Constitution should provide protection from the discriminatory aspects of culture.

Kuwe na two national languages, English number one and then Kiswahili.

The Constitution should recognize indigenous languages but not promote them. Pesa za umma sizitumiwe to promote indigenous languages maanake ukizaliwa katika kabila ya... kama wazazi wako wana kabila watakufunza kabila yako.

Management of natural resources. All parastatals employees should have uniform scales unlike today. All parastatal boards should have uniform scales of payment unlike today where some parastatal their scales are very much higher than those of other parastatals and yet those employees they are public servants and whatever they are doing they are building the nation. It is very hard to understand why a messenger in Central Bank earns more than a graduate teacher, very hard to understand. Yangu ni hayo.

Com Salome: Asante sana Bwana Kitimbi.

Paul Kitimbi: Nilitoa maoni Tononoka lakini hizi sehemu ambao nimeguza leo they were not included, nimeongeza.

Com Salome: Sasa nimuite Abdalla Moi.

Abdalla Ali: Waheshimiwa mliokuwaq hapa mabibi na ma bwana na Tume ya kuandaa marekebisho ya katiba hamjambo. Nia na mathumuni ya mimi kusimama hapa ama kuzungumza mbale yenu, naona mengi yamezungumzwa kuhusiana na polisi lakini mimi ninazungumzia zaidi na nina iomba. Mimi ninaitwa Abdalla Ali Moi as a Mombassa comedian, asa a founder comedian. I am a commentator of this Tume ambayo tunaendelea nayo.

Ninazungumzia juu ya vijana kwani watu wote wamezungumzia kuhusu mishahara, kuhusu kazi lakini si vijana wa leo na maisha ya baadaye. Ningeomba Tume hii ya marekebisho ya katiba itilie maanani kuhusiana na vijana. Ninalia wivu sana mimi kama mkaazi wa hapa Mombasa, definitely as a founder comedian, street comedian na mpaka nikaweza kufika jina na I can imitate about 30 language, naweza ku-imitate. Ni kwamba wakaazi wa mkoa wa Pwani they are challenging lakini naomba Tume ya marekebisho hii ya katiba itilie maanani kuhusu vijana kwani utakuta upande wa uvutaji bangi Mombasa, Vipuli sijui wapi wote from Mombasa. Yote inatokana ni kwamba when you are looking for this Girl Guide wa Bora scouts they are well smart. If you

are looking for this Kojia community they are well smart, but if you are looking for our Mombasa six Arab Scout wakuta mwingine amevaa chapali, mwingine vilemba vimekwenda juu, mwingine amevaa suruali ya cowbow. Vijana wale wale they are best swimmers, vijana wale wale wengine wamesomea mambo ya first aid, leo dani ya Makadara ninatumai hamjawai kufika na Mungu atajalia nitawaalika mimi mwenyewe rasimi mje mutembee kwenye Fan Fair Except Stadium ikiwa kuna mechi, utakuta ambulance na first aid iko pale. Lakini ikiwa kuna sherehe zingine ambazo ni muhimu basi uwezi kukuta ambulance iko pale, uwezi kukuta scout girl guide ako pale na leo ikiwa vijana wale hawakutupiwa vijizi because if anything kesho watapata kazi navy, watapata kazi kwenye serikali na mahali penginepo. Ningeomba Tume hii itilie maanani na izungumzie swala la vijana kwani katika mkoa huu wa pwani ni mziki wanasorota. Natumai wageni wetu wa heshima kutoka mlipokuja last time Tononoka si kuja nilisikiza lakini this time nikajitolea rasimi kufanya public address na mwenyewe nije nizungumza.

Mumeona namna machokora, ikiwa hatutakuwa na mahali kiwanja tunapewa hall we train them kutakuja mambo ya swimming, navy watatusaidia, katiba itatusaidia mpya ambao itakaotungwa na tutaweza kuwafukuza watoto hawa baadaye some of them they will be simulitonic, watakuwa na sehemu mbali mbali. Leo ukificha uhuru na kazi, gari za serikali hazipungui hamsini ziko pale. Tuna wafungwa ambao they are in prison those who can make those cars na zitafanya kazi. Kwa hivyo naomba Tume hii ituwezeshe sisi vijana.

Mimi ni mmoja ambaye pia ningependa kuzungumzia jambo la pili. Upande wa wizara wa utamaduni, Tumewekwa nyuma sana, hatuna human rights. Katika Kenya leo maoni yangu ninayatoa mbele ya kamati hii ambayo iko hapa kusikiliza maoni yetu. Mimi kama Abdalla Ali ambaye ndio mwanzilishi katika Mombasa mchezo wa kuigiza, sauti na kufanya mengi. Leo Redycluss wanafanya na cassettes zinazwa kila mahali. We don't have human rights, Kenya hatuna. Leo nitachukua cassette ni muazime huyu, huyu atakwenda atamwazima yule ata- record-iwa hapa. Chukua hii ya Mtanzania, they are coming soon, wacha wakushike na hii cassette you won't believe it, you will pay the fine na watakushitaki vile iunavyotaka. Ningeomba sisi wasanii, Kenya hatutambuliwi.

Mr. Coast where is he, Mzee Mombassa, leo mzee Mombassa na taalibu sister. Nyumba ya kuangaliwa ambapo wa Kenya wako, Waislamu wako, communities ziko ambazo ningeomba Tume hii iweze kuwasaidia wasanii kama sisi. Natumai mliposikia Abdalla Moi mliona nitakuja na Benzi, mkimuangalia hata baiskeli hana, yote ni kutokana na haki za wasanii wa Kenya. Tembea barabarani utakuta kasheshe ni msanii, magazeti kutoka Tanzania ya wale wanasanii.

Promoters, maunivu yameimba siku za kuimba jana na juzi ndio utaona cassette yake inapita hapa. Kwa hivyo naomba kamati hii itilie mkazo kuhusiana kwanza kuhusu hao vijana tuunde kamati. Mimi I am ready to be a leader na nitawaita wengine tuongozane ili vijana hawa, and I am 100% tembea na gari utakuta wasimama mimi mwenyewe nawaita waiting for the bus which has not come. Waangalia huku na huku wafikiria wangoja basi mpaka saa kumi na mbili. So njia ya kuondosha ugonjwa ule when we keep them busy everyday. Kuna wale ambao Tumeshidwa na vilema walioko Likoni. Wanaweza kuimba a national anthem na kila kitu na si kwamba viombo hivi Kenya girl guide scout haina, they have lakini Kisauni constituency ward

hii imetupwa kabisa. Nazungumza kwa niaba ya vijana wote wa Kenya kwamba ukithibitisha na definitely kuna wale ambao pia first aid kuna wengine ambao wana elimu zao lakini ukiwaangalia suruuri zina tundu kwa barasani. Salamaleku mdosi, kutoka asubui mpaka saa kumi salama maleku. Kwa hayo machache sina mengi ya kusema na kesho tutakapokuwa pamoja nitazungumza mengine ambayo ningeomba Tume hii ambayo imekuja hapa kutusikiliza sisi itilie maanani haswa kuhusu sisi wasanii. Tutatoa cassette kwa ajili ya kutekesha kesho nitategwa mimi naona hapa. Kwa hayo machache asante.

Com Salome: Asante sana Abdalla Moi. Ambaye anafuata ni Abdalla Baghazala.

Abdalla Baghazala: Jina langu ni Abdalla Baghazala very simple and very romantic. Lengo langu la kuja hapa ni kutoa maoni yangu kwa Tume hii juu ya vijana ambao wametajwa mara nyingi, youths. Mpaka sasa na katiba hii tunayo hapa hakuna pahali popote inaposema vijana wale ambao walioleta sifa katika Kenya kwa njia ya michezo ya aina yoyote watazamwe, wajulikane na wapatiwe nisani katika nchi.

Waalimu waliotengeneza vijana wakawa wanaki vizuri uleta sifa ndani ya nchi. Wale waalimu wao vile vile watabuni kali. Nina kuhakikishia maanake mimi nimesafiri nchi nyingi, vijana wetu wengine wanajinyima harafu duniani kwa michezo kuliko mawaziri wetu wengine dani ya Kenya na wameleta sifa nyingi sana. Sitaki kutaja majina maalum, tizama riadhaa utaona katika riadha ambao mimi sikuja kama mwana chama wa mkoa wa Pwani ambao mimi ni mmoja wapo lakini mapoja kutoa maoni yangu wanajulikana zaidi ya wajumbe wetu Kenya. Mimi nimekwenda nao kama kimeneja, watu hawakujui. Wasema Kenya iko wapi, mmoja wamuambia iko West Indies lakini hawa vijana wetu wanaleta sifa kubwa. Tulikwenda Greece tukaulizwa inatoka wapi tukasema tunatoka Kenya siku hizo, Oh! Kenyatta Keino. Kenyatta na Keino, unajua wanajulikana wa quality, Kipchoge Keino na Kenyatta. Kwa hivyo mimi ninaomba very seriously Ministry of Sports should be amalgamated with the Ministry of Tourism kwa sababu vijana hawa timuzi wetu za leta sifa kubwa sana wakicheza, wakikimbia inje ya nchi yetu na tukiendelea hivi hivi bila mipango maalum unakuta nchi inaongeza uchumi ambao shida yetu kubwa ya Kenya leo ni uchumi. Hata jana World Bank inasema bado hatujarekebisha mambo, hatujui ni mambo gani tutarekebisha tena. Njia moja ni kuleta watalii na tunaweza kuleta watalii tukileta the Ministry of Sports na Ministry of Tourism pamoja, uenda mipango yetu yakuta nchi yetu inje itajulikana sifa zaidi kuwa watu wasione kuwa Kenya ati mambo ni mabaya, mambo si mabaya hivyo tunavyofikiria. Kuna nchi nyingi ni mbaya kweli kuliko kiti. Hilo ndio onyo la kwanza, maoni yangu ya kwanza ya kufikiria youth na kuwa amalgamated.

La pili ningeomba ingawa limetajwa lakini mimi ninataka kusisitiza tu lisemwe zaidi kwa sababu kila jambo likisemwa huyu na huyu na huyu na huyu Makomishona mtasema hapa hakuna jambo. Kuchaguliwa kwa ma mayor katika Kenya; kuchaguliwa na ma- councilors peke yake ndio shida kubwa tunayo leo katika Kenya habari ya mayor kwa sababu ni kidogo na watu kidogo kila siku unaweza kuzungumza lakini wacha wananchi wamjue yule, wachague mayor kama vile wanavyochagua councilor. Isiwe mambo ya ward, ward yako kule inakotoka haitoshi lakini iwe ni mji nzima inamchagua mayor. Sababu(inaudible) huyo mayor haitakuwa kwa councilor. Sasa yeye anasikiza councilors maanake ndio waliomchagua lakini kama wananchi wamemchagua inakuwa lazima sasa asikie wananchi. Wananchi hawana njia yoyote ya

kumuambia mayor Tumekuchagua sisi labda ward yake ndio itamuambia sisi Tumekuchagua kuwa wewe ni councilor. Na wale ma Chairmen walioko ndani ya council vile vile wale wachaguliwe na wananchi wa mji huo. Mayor wa mji awe atoka katika mji ule ule, anazijua shida za watu, anawajua watu wenyewe, anawajua historia yao, ndio atajua na atafanya kazi yake kwa uzuri. Kwa hayo machache ninawashukuru kwa kunipa nafasi hii na nakoma kama kuna maswali yooyte, comments niko tayari kujibu.

Com Salome: Asante sana Bwana Abdalla. Kuna swali kwa Abdalla.

Com Wambua: Umesema kuwa mayors wawe wanakuwa elected lakini sio na ma councilors na mayors na Chairman wawe wanatumikia watu wote kwa ile mji. Kwa hivyo ningependelea kujua kama ni maoni yako kwamba mayor na Chairman wasiwe na ward ambao wanasimamia. Kama wanataka kuchaguliwa kama ma chairmen ama mayor asiwe na ward Fulani. Wachaguliwe na watu wasimame kitu cha mayor wachaguliwe na watu wote ama kwanza atasimama kama councilor halafu achaguliwe kama mayor. Ungependelea namna gani kwa maoni yako kuhusu hiyo jambo.

Abdalah Baghazala: Lengo Kubwa ya kurekebisha katiba, lengo kubwa ni kurahisisha mambo yasiwe magumu zaidi. Kwanza kwa mambo ya fedha, hatutaki duplication na taabu. Mwanzo lazima upate, uwezi kuwa mayor kabla ujawa councilor, uwe councilor watu wako wakuchagua wa mtaani lakini si wale ma councilors wengine wa kuchagua wewe uwe mayor. Uwe councilor kisha Councillor ma Chairmen na mayors wachaguliwe na ule mji. Kama ni Kilifi, kama ni Mombasa iwe ni Mombasa na may the best man win. Nimejaribu kukjibu.

Com Salome: (inaudible).

Abdalah Baghazala: Nakubaliana na yeye lakini modalities zao tuachie Electoral Commission wafanyi. Kuna Commission kama nyinyi ambayo inachunguza mambo ya uchaguzi. Mimi ninasema wachaguliwe na Wananchi. Sasa vipi watakoachaguliwa ni vipi sasa hizo ni modalities, technicalities zenu nyinyi na Electoral Commission watasaidia. Nchi nyingine wanafanya hivyo, sisi hatutakuwa wa kwanza katika ulimwengu, wa mayors kuchaguliwa na watu maanake ukisema hivyo, nimekwenda Scandinavia nimeona mayors wanachaguliwa na Wananchi na ma mayors wote ndio Chairmen kwa parastatals, zile strategic parastatals ndio ma mayor.

Com Salome: (inaudible).

Japhet Muinga: Kwa majina yangu ninaitwa Japhet Muinga na nimzaliwa wa hapa mji huu. Kwanza ningeanza na uchaguzi wa raisi ama uchaguzi wa wa Bunge wetu, ya kwamba kungekuwa na siku mbili tofauti, siku ya kwanza tuchague wa Bunge wote halafu baadaye ndio sasa kuje kuwe na uchaguzi wa raisi.

Pili ni kwamba huyu rais awe sasa abaweza kuchagua Prime Minister na hizi parastatals zote, wale the heads of parastatals

wawe wanachaguliwa na committee za Bunge na ingekuwa ni hivi. Ya kwamba ikiwa ni parastatal kwa mfano kama KPA, nafasi itolewe itangazwe ya kwamba kunatakiwa Chairman wa KPA. Watu wajitokeze kwa majina halafu ku-formiwe special committee ya parliament ambayo ita interview hawa watu ambao wangechaguliwa. Halafu wale watatu ambao wangechaguliwa ndio sasa wapelekwe kama ni Bunge ama ni kwa raisi waweze kuwa appointed mmoja lakini raisi asiwe na mmalaka maalum ya ku-appoint mtu, kwa mfano kama vile inavyotendeka habari za saa saba unasikia mtu amechaguliwa na ameondolewa muda fulani.

Nikirudia hapo nyuma, huu ni wakati ambapo tungejivunia ama tungekula matunda ya elimu yetu ambayo Tumejifundisha kwa muda huu miaka thelaqhini. Kwanza kungekuwa na viwango maalum, rais wa nchi awe ni mtu aliyesoma na awe na kiwango kama ni cha professor, yaani ninamaanisha ya kwamba kuna watu ambao wamesomea political science na nina amini ya kwamba watu kama hao ni watu ambao wakipewa nafasi katika nchi wanaweza kuiongoza vilivyo maanake n hiyo ndio area ambayo walikuwa wakosomea. Kwa hivyo kuwe ni watu ambao ni wajuzi wamesomea upande huo kwa mfano kama professor na hawa wa Bunge ambao dani yake kutapatikana ministers wawe ni watu wa degree minimum, wawe na degree moja. Hivyo unaweza kupata kama ni minister wa education ni mtu ambaye ni professional katika education amesomea education kwa kiwango kile cha degree level kama ni minister wa health ni health ni mtu ambaye ni dakitari amesomea eneo hilo lakini tusichukue dakitari halafu tunamuweka awe minister wa cooperative development.

Hiyo ni makosa ma kubwa tunachanganya. tunachukua watu ambao wamesomea eneo lile na anawekwa mahali pale. Halafu appointment of ministers inakuwa ni kwamba hizi ministries kwanza wale viongozi wa ministries wanakuwa ni watu wanaochaguliwa kama vile nilivyo sema kwa hizo parastatals. Watu wanachaguliwa na committee ya Bunge ku head hiyo ministry yote, yaani yule tunamuita permanent secretary awe pia naye anachaguliwa kutokana na committee ya Bunge. Halafu yule anakuwa ndio chairman wa permanent secretary. Minister anachaguliwa na raisi lakini sasa huyo minister na permanent secretary ndio ambao sasa wanaendesha hiyo ministry na ikiwa kuna swali lolote kuhusiana na ministry hiyo basi inakuwa ni raisi kuuliza yule mtu ambaye amechaguliwa na Bunge na kufutwa ni rahisi kufutwa na Bunge. Hiyo ni kuonyesha kwamba mamlaka ya raisi, kuchagua permanent secretary pasiweko. Mambo mengi sana yawachiwe bunge ama ningesema kwamba Bunge lipewe mamlaka zaidi kuliko raisi maanake raisi ni mtu mmoja. He can easily be manipulated, hatuwezi kusema mimi ndio nilimchagua mimi ni rais mimi nitakuwa more genius than any other Kenyan. I can always be manipulated here within or even outside the country. Naweza kuwa na outside forces, they may be other super powers wakanilazimisha mimi kama mtu mmoja kugeuza manno ya nchi yetu lakini ikiwa Bunge letu ndio lenye mamlaka zaidi kuliko raisi inakuwa sio rahisi kumliki mambo yote maanake ile ni Baraza la wazee na ikiwa kuna jambo lolote ambalo linahusu serikali inabidi kwamba lile lipitishwe na Baraza la wazee. Wawe ni presentatives wametoka area fulani fulani za nchi walioheshimiwa kwa hivyo wana haki kusikizwa katika maoni.

Jambo lingine ni kwamba hawa wa Bunge wawe na ofisi maalum ambazo Wananchi wanazitambua kwamba hii ni ofisi ya Mbunge wao. Kama hivi sasa unafanya kubahatisha hujui ofisi ya Mbunge wenu iko wapi na hata ukiwa na maoni ujui uende

wapi. Kuwe na ofisi maalum, institutions ambazo zimejengwa kwa mfano kama hii Chandaria Hall ama hii area tujue hapa ndio ofisi ya Mbunge wa Mvita na haijalishi kama ni wa chama gani. So long as wewe ni Mbunge wa Mvita atakuwa na right ku-assume hii ofisi na akiondolewa kuwa Mbunge wa Mvita ana-vacate office na hapa kunakuwa na hall kama hivi ambapo kuna siku maalum Wananchi wenyewe wanaweza kuja wakajadiliana juu ya mswada ya nchi ama juu ya jambo fulani maanake Sheria nchi inanza kutokana na Wananchi wenyewe. Tunapokaa hapa na kujadiliana juu ya msaada fulani wa eneo letu hapa tukiwa na councilor wa eneo hili ama wazee wa mtaa huu hapo ni rahisi kuandika ule mswada ama memorandum tukampatia Mbunge wetu kwa kusema sisi kama wakaazi wa Mombasa Tumekaa na tukasema kwamba jambo hili twataka wewe ndio ukalijadilie Bungeni. Kwa hivyo hili ni jambo ambapo Mbunge wetu akiwa kule Mbungeni na sisi tutakuwa tuna radio tunasikiza, tuna TV tunaangalia maanake ni kitu Tumemutuma na hatakuwa yeye mwenyewe ametuma maneno yake.

Lakini vile ilivyo unakuta kwamba un less Mbunge yeye mwenyewe awe novative utamsikia kimbelebele kule Bungeni. Wa Bunge wengine yeye ameenda kule lakini hana mjadala unaweza kusikia Mbunge amekaa kule miaka kumi na tano miaka ishirini hajaletaa mswada hata mmoja lakini wakati wa kura ndio unamuona yuko active kwa hivyo kila constituency iwe na office ya Mbunge wake ambayo itakuwa inaweza kutambulikana.

Nikirudia kwa upande wa wafanyi kazi, wafanyi kazi tunabaguliwa sana kwa upande wa taxation, utakuta kwamba wengine wanakuwa over taxed than others. Kuna watu wengine hata hawa-tax-wi kabisa, wanaishi tu humu humu. Halafu hii tax nayo kwa wale ile group ya watu ambao wana tax-iwa nayo wamenyanyaswa. Utakuta kwamba mfanyi kazi wa serikali kama minister ama mfanyi kazi wa serikali tuseme, mshahara yake waweza kuwa 30,000 shillings na ana post kubwa sana kule serikalini lakini mshahara wake waweza kuwa elfu thalathini. Sasa hii Sheria ilioko ni kwamba wana tax mshahara ile inaitwa salary, wana-cut salary. Lakini kuna hizi zinaitwa fringe benefits ama allowances, haya mambo mengine haya tax-wi mtu anapewa kamili, kama nyumba anapewa kamili, kama ni gari anapewa kamili, mafuta vitu hivi vingine kama ni kusomeshewa watoto atasomeshewa kamili. Sasa utakuta mtu wa serikali saa hii salary ni kidogo kama elfu ishirini. Ikifika taxation kama ni 20% ina tax-wa ile ile 20% of of the 20,000 ambayo inakuwa ni elfu nne. Lakini mtu yule yule na fringe benefits anapewa elfu sabini ama anapewa elfu themanini. Sasa unakuta kwamba huyu mtu wa serikali, uwezi ku-imagine mtu wa serikali ambaye anapata pesa kidogo kiasi hicho na mtu mwingine wa kazi ya kapuni ya kawaida ambaye anapata the same amount. Ni kwanini huyu anakuwa na pesa ntingi ama anakuwa na mali nyingi kwa muda kidogo kuliko huyu mwingine, ni kwa sababu ya zile fringe benefits. Sasa sisi wafanyi kazi wa kawaida tunapewa mshahara mkubwa lakini sasa sometimes little allowances or no allowances at all ama fringe benefits. Sasa ikija ikifikia taxation we become the sufferers, we earn less than hao wengine. Kuna areas zingine kuna group za watu wengine ambao hawa tax-wi kabisa. Kwa mfano kama farmers, watu wenye nyumba za kukodisha kama hizi za elfu mbili na below, watu wenye Matatu. Ninatajia tu lakini kuna watu wengine nasema kwamba hawa tax-wi kabisa kwa hivyo taxation imekuwa iko juu sana.

Halafu nikija upande wa kwa mfano kama madereva,. Unakuta kwamba dereva ana-cause accident na dereva huyu huyu anaruhusiwa kuendesha gari tena. Dereva mmoja naweza ku-cause accident mara tano mara sita. Ingekuwa kwamba dereva

aki-cause accident kama amaeuwa anyimwe hiyo licence kabisa, asiruhusiwe kuendesha gari tena. Kama ni public vehicle ameenda amependua na wamekufa watu kama sitini huyo akatazwe. Ikiwa ni dereva ambaye ameumiza watu, lakini drivers from time to time wapewe nafasi tena warudi tena for re-checking wa- test-we tena waone kama anaweza kuendesha gari ama la. Halafu nikija kwa upande wa kama hiyo area kwa mfano kalma farmers ningependa kwamba hii agricultural institutes ziwe open to everybody, sisiwe kama ni watu ambao wamemaliza skuli, ama watu ambao labda wamekosa kazi, wametafuta kazi wamekosa ndio wanaenda huko halafu wanakuwa extension farmers. Halafu wakiwa extension farmers wanakuwa dis-interested they don go. In this case ingekuwa ni kwamba vyioo vya agricultural view open to every body na kila mtu akienmda akisoma pale tayari anaenda shambani ana-purchase, serikali ita-save mshahara ya kuandika extension farmers na pili farmers wetu watakuwa professionally trained. Saa hii farmers wetu wanabahatisha bahatisha, lakini tunataka profession farmers.

Com Salome: Asante sana Bwana Muinga. Kuna swali kwa bwana Muinga?

Com Pastor Ayonga: Nilisikia ukisema kwamba mara nyingi awe amesoma na (inaudible)

Com Wambua: (inaudible)

Japhet Muinga: Asanteni. Kwa ajili ya swali la kwanza mimi ninaamini ya kwamba kuna wasomi wengi ambao wako nje ya nchi yetu haswa zaidi ma professor amabo wangukuwa hapa nchini wangukuwa encouraged wanaweza kuendesha mambo vilivyo. Lakini wameangalia hii situation wakaona badala ya kungangana ni heri wakatafute kazi nje. Pili ni kwamba ikiwa kama mimi kwa mfano nimesoma vilivyo kwa upande wa administration na professor ni mtu ambaye hata nimesoma na nime-practice or hata pamoja na kwamba kuna ile akili ya kuzaliwa lakini hili ni jambao ambalo nimelosomea na nimehitimu katika upande huo. If I was a successful manager and specially up to that level it means that I can run the country well. Kuliko kama mtu ambaye labda hakuwa amesomea area hiyo.

Kujibu swali la pili ni kwamba hawa wa Bunge isiwe kwamba watu wanachaguliwa kutokana na ile the winning party peke yake. Ikiwa kwenye winning party amekosekana mtu wa daraja lile, basi lazima tuwe tayari kutupa macho katika the opposition party pia napo tuangalie. I am sure out of hao wote haiwezekana, itakuwa very little chances kwamba tutakosa mtu ambaye anaweza kushikilia ile position kabla hatujaangalia any other alternative and especially ikiwa the permanent secretaries ni watu ambao walikuwa na kiwango kile, huyu minister is only a chairman to the board unaona. A chairman kazi yake ni just to conduct a meeting lakini here we have got a permanent secretary who is a secretary to that ministry. I am sure that ministry can run very well.

Com Salome: Asante sana Bwana Muinga, jandikishe pale. Anaye fuata huyo ni Muniri Masudi.

Muniri Masudi: Jina langu ni Muniri Masudi. Ma- Commissioner wa Tuem hii mabibi na ma-bwana salama maleku? Yangu yatakuwa mafupi kwa sababu nilikuwa sikupanga kuja kuzungumza leo lakini nimeona nafasi ilioko nitumie nafasi hiyo. Jambo la kwanza, ningependa kuzungumzia Katiba yenyewe kile kitabu chenyewe kilivyo. Ukitazama katika Katiba yetu ya Kenya ni kama iko naked tupu. Nimewai kupata bahati ya kuona Katiba moja, Katiba ya Uganda ambayo ina kitu kama preamble au maelezo ya kueleza nini watu wa nchi ile wanataka katika Katiba yao. Kwa ufupi lengo la ile Katiba ni nini? Kwa hivyo ikiwa tunaita Katiba ni Sheria ya mama, sasa kuna mama wa ile Sheria ya mama yale malengo ama maono ya watu, vision yao wanataka Katiba yao iwafanyie nini, iwapeleke wapi. Ina maana kwamba ikiwa Katiba yenyewe kutakuwa na kifungu chochote ambacho hakikutosheleza matakwa ya wananchi⁹ wenyewe basi ile Katiba yenyewe itakuwa ina upungufu na wakati wowote itakapojulikana mbeleni, inatakiwa irekebishwe ili iambatane na matakwa ya Wananchi wenyewe.

Jambo loa pili kuhusu Katiba ningependa kwamba mpango huu uliopo wa marekebisho ya Katiba usimalizike baada ya hii shuguli yenu. Iwe ni kitu continuous kwa sababu ukitazama ndugu zetu wa Uganda ambao nafikiri Katiba yao ni mara kumi, utanisamehe ikiwa nimekosea, ni mara kumi bora kuliko Katiba yetu ya leo. Katiba yao ya pili walio ibadilisha baada ya ile walio irithi wakati wa ukoloni ninaiona ni mara kumi bora kuliko yetu lakini muda wa miaka mitano baada ya kuitengeneza hiyo Katiba nzuri, tayari wameshaona matatizo ndani ya Katiba hiyo na wanataka hivi sasa wanaifanyia marekebisho tena. Kwa hivyo tungeomba katika Katiba hii itakayotengenezwa sasa, iingizwe ndani yake kifungu kwamba itakuwa ni continuous process, utengenezaji wa Katiba. Vipi itafanyika namna hiyo ni nyinyi mtaangalia na wajuzi wengine.

Jambo lingine ambalo ningependa kusema kuhusu Katiba ni maoni ya Wananchi ambayo yatapokelewa sasa. Ikiwa Katiba hii kweli itakuwa, basi maoni hayo hayafai kupingwa na ma-agent ya Wananchi wenyewe. Nikisema ma-agent ninamaanisha wa Bunge wetu. Kwa heshima ninachukulia kwamba wa Bunge ni ma- agent ya Wananchi wanakwenda kuwaaki⁸lisha. Ikiwa leo Wananchi wenyewe wamesema, sidhani kwamba agent ataweza kusema kinyume na wenyewe walivyo sema kwa hivyo tanaomba kwa heshioma Bunge likubali kwamba maoni yatakaopitishwa na Wananchi wa Kenya wao watakuwa ni kuwapigia rubber stamp peke yake. Ikiwa watakuwa wameona tatizo lolote, kuna upungufu wowote, basi wairudishe kwa Wananchi wenyewe, wawaambie kwamba Tumeona kuna upungufu fulani na Wananchi wenyewe waamue wangependa kurekebisha jambo hilo namna gani. Sio wao kama ma- agent wa Wananchi kwenda kubadilisha na wakaleta kitu kingine ambacho wananchi wenyewe hawakufikiria.

Sasa napenda kuzungumzia kuhusu chama cha KOTU. Chama cha KOTU kinawakilisha wafanyaji kazi, na wafanyaji kazi ndio utu wa mgongo wa uchumi. Bila wafanyaji kazi hatuwezi kuwa na uchumi na wala hakuwezi kuwa na nchi yoyote. Kuna matatizo kwamba wafanyaji kazi haki zao zinapuuzwa kwa sababu ya chama kama cha koti bila umbrella organization uwa kimekuwa cubed ama kimekamatwa ama kinatawaliwa na nguvu nyingine ambayo ni nje ya wale Wananchi. Tungependa basi mwenyekiti ama secretary wa general wa KOTU awe ni automatic member of parliament katika Bunge lolote lile ili asiwe na hamu ya kutaka, secretary general asiwe na hamu ya kutaka Ubunge, akaenda kuomba vyama vikamfadhili kumsaidia kupata Ubunge kisha akawauza Wananchi wote wafanyaji kazi ndani ya siasa ya vyama vile.

Kwa nukta hiyo hiyo, ningepeda pia wale wa Bunge wanaitwa nominated member of parliament. hawa wanakula mishahara mikubwa sana pesa za Wananchi na hii Wananchi wenyewe wameshachagua watu wao waakilishi wao. Haifai nominated seats ziwe zinapewa zawadi ya vyama wamutumikie mtu ambaye wanaempenda. Zile lazima ziwe for specific purpose, ikiwa ni public interest, iwe ni public interest, sio interest ya chama au ya mkuu wa nchi au mkuu wa dollar. Kwa hivyo kuangaliwe namna nyingine ya kutumika hivi viti za member of parliament sio wanaganyiwa nyinyi mko watu hamsini mtapata viti fulani, angalieni girlfriend wako, angalia bwana wako, angalia hivi, nafikiri hiyo nikuharibu mali ya Wananchi kwa sababu watu wale hawalipwi na vile vyama wananlipwa na pesa ya Wananchi. Ikiwa watapewa nominated member of parliament kama civic society apewe kwa mfano ndugu yangu alivyosema kumekosekana dakitari, apewe ni doctor au kunakosekana architecture apewe Law Society of Kenya chairman wake apewe zile nominated. Utaona kwamba hii ni pesa nyingi ambazo wanakula na Wananchi wengi wanajitolea kazi kwa mfano PTAs katika maskuli wanafanya wakati Mwingi sana lakini hakuna mtu anayewalipa committee members katika PTA. Dani ya Bunge wanalipwa sijui ni laki nne wengine anasema ni laki sita, na yeye ni nominated member of parliament na haendi katika Bunge mpaka business ya Bunge inasimama kwa sababu hakuna forum. Sasa ile zawadi walipewa Ilikuwa ni ya kazi gani. Kwa hivyo jambo hilo lisiwachiwe wa Bunge kuamua. Liingizwe katika Katiba zili wa Bunge wasiende kulibadilisha tena.

Naomba kuzungumzia kuhusu chama kinachoitwa kwa kingereza NASADA (National Agency of Campaign Against Drug ABUSE). Nafikiri chama hiki kinaoongozwa na ndugu Joseph Kaguthi. Hatujui ni kutokana na shirikizo kutoka serikali za nje au mashirika ya nje iliyo ilazimisha serikali ya Kenya ikaamua kuanzisha hii NASADA, hatujui lakini Kenya ilikuwa inapotea katika mambo ya madawa ya kulevyia na ni business kubwa sana na ni wazi watu wenye kufanya biashara hizi wanajulikana, ni watu wana connection na watu wakubwa. Siku moja tukasikia katika KBC kutoka state House kumeanzishwa NASADA. Ina maana kwamba kesho KBC ile ile inaweza kutangaza kwamba Joseph Kaguthi rudi zako nyumbani. Hatukujua alipewa Kaguthi labda ako kabla fulani inataka kurudishwa karibu nasi, hii ni kisiasa au ni vipi, au ni kweli inataka kushugulikiwa tatizo la madawa ya kulevyia. Ikiwa ni hivyo basi tunasema hivi, NASADA ingizwe katika Katiba kama ilivyo Attorney General office and tenure of office ama audit and controller general ama office nyingine. NASADA iwe pale na Mbunge ama Bunge ama mawazsiri ama raisi hawezi kumungoa. Na tungependekeza kwamba Joseph Kaguthi ikiwa hatawekwa yeye anafaa katika hiyo kazi. Tunasitikiza kwamba Kaguthi anatembea Kenya nzima akiulizwa unaweza kufanya nini kuhusu madawa anasema mimi ziwezi kazi yangu ni kuambia watu basi wachni wacheni kwa sababu amepewa huku jukumu la kufanya pesa nyingi wakati mwingi lakini hakupewa authority au nguvu, uwezo wa kuzuia kwa sababu anajua wenye kufanya na binu wanazo fanya zinajulikana lakini anashidwa kwa sababu amepewa na amepokonywa.

Naomba kuzungumzia kuhusu judiciary idara ya mahakama. Nafikiri wa Kenya wengi wanakubali kwamba mahakama zetu zimeshindwa na kazi kwa heshima na nafikiri niko na protection nisije nikatoka hapa kesho nikatafutiwa huko nikaenda nikatupiliwa mbali sijui wapi. Kuna kesi katika mahakama ziko miaka tisa na ma judge wamepandishiwa mishahara na hawa wanasumbua watu mtu unaweza kupelekana na mwenzio kotini mpaka mtu akafariki kesi hazijamalizika na kesi wanazozitaka

siku mbili. Juzi mayor wetu wa Mombasa ameshikwa leo ametegwa kotini. Mimi nina kesi bibi yangu alishikwa miaka saba mpaka leo haijasikizwa. Mahakama zenyewe ukifika pale hatutambui tuko Kenya ama tuko London kwa sababu Sheria zilioko katika mahakama ni Sheria ambazo mwamnachi wa Kenya hazielewi. Mahakama ambayo ingefaa iwe inafanyika London ndio iko hapa Kenya Mombasa. Kwa nini tuhukumiwe na Sheria za mwiingereza. Sheria zenyewe ni mbovu hazitufai, judge anaweza kuamua huyu mtu ameiba watu wote wamemuona ameiba wazi wazi na akiasema huyu akuna kesi aliyehitimu au wakili wake amekosa kuleta karatasi fulani kwa hivyo huyu kule kuiba kwake kwote kumekuwa si kuiba tena. Kwa hivyo sheuria ni mbovu wenye kuzipeleka ni wabovu, nafikiri ma judge wenyewe wamewai kusema moja Kwach kwamba kuna corruption akaihtwa mbio akanyamazishwa azizungumze lugha hiyo. Kuna corruption, sheri a zenyewe zinazotumika pale hazitufai nafikiri ingekuwa bora. Pmahakama zetu za kienyeji zipewe priority kwanza ambaye hataki kuhukumiwa kwa Sheria zetu za kienyeji ndio achague kwenda katika mahakama zao za wazungu.

Jambo la mwisho ambalo ningependa kuzungumza ni kuhusu ukabila. Bwana mwenyekiti wa kamati hii, tunamsikia kiongozi wa jamuhuri yetu kwa heshima kabisa akizungumza Kenya hakuna ukabila, mimi sitaki ukabila lakini mambo practically yanaofanyika on the ground ni ya ukabila mtupu wazi wazi. Sasa twaomba Katiba hii iangalie binu kuondosha huu kwamba hakuna ukabila na ukabila twauona upo. Nyinyi kama experts mukae na wengine mtafute vipi tutatutua tatizo hili. Mimi ningependa kwamba tukubali kwamba ukabila uko na tu-institutionalize kisha tugawanyiane kulingana na yale makabila nafikiri tutakuwa pale, tutaweza kufanyana haki kuliko kusema hakuna ukabila. Ukiingia ofisi ya moja kuanzia juu mpaka mwisho watu hamsini wote ni kabila moja na wengine watakwenda wapi. Hatukatai, tunataka tuchanganyike kabisa, mix. Kenya yote ni ya wa Kenya wote na kuna nafasi kila mtu apate, lakini mwingine akisha kuingia pale juu basi hakuungiimwingine kule. Ni shemeji yake, ni dada yake, mjomba wake, nani wake, ni makosa. Kwa hivyo tungesema hivi tukubali kwamba ukabila upo na kila mtu ana kabila yake kisha tukae chini tupangiane. Halafu tukitaka kuondoa ukabila yale makabila yenyewe yaweke waakilishi wao wazungumze tutaondoa vipi ukabila. Watakapo kubaliana tutaondisha, kabila hatujakubaliana tuukubali upo na uwekwe katika Katiba na mambo yote yaende kulingana na quarter ili kila mtu apate ile keki inayoitwa Kenya. kwa hayo machache ninatoa shukrani sana kwa kamati hii. Sikuwa nimejitayarisha lakini nikaona nafasi iko nikachukua nafasi hiyo pengine kesho tutakuwa na watu wengi zaidi.

Com Salome: Asante sana Muniri Masudi. Kuna swali kwa Bwana Muniri.

Speaker: (inaudible)

Muniri Masudi: Ma-Commissioners kwa ruhusa yenu alivyo sema ndugu Abdalla kwanza kwamba the Constitution itarudishwa kwetu inaweza kuwa kweli lakini baada ya hapo mwisho wake itarudi parliament kwa adoption nafikiri. Sasa ni wakati ule ambapo wale jamaa zetu waheshimiwa wanaweza kui-doctor wakaifanya wanavyotaka ndio ikapita sisi twasema wakati ule ndio wasiiguze tena. Hivi sasa wao kama Wananchi wa Kenya pia waweza ku-contribute kama mwingine lakini wakati ule wakati wote Tumekubaliana ndio hivyo. Ikienda pale kwao katikak parliament wasiwe na kuibadilisha tena, ni hiyo

nilikuwa nazungumza.

Kuhusu makabila watu ambao hawajui labda kabila gani, kwanza tutakuwa na zile main tribes kisha halafu wale watu hawajui basi watachukuliwa the nearest tribe ama vingine ama wale experts wataonyesha ni namna gani. Lakini wale ambao wanajulikana wazi na hatufanyi kwa sababu tuna-bias against tribes, no. Tuna respect kwa sababu ni kitu cha Mungu ndio alipanga namna hiyo, lakini nataka tuwe na justice na fairness. Tunatafuta viti tutapata justice na fairness kwa sababu miaka thelathini na saba tangu tupate independence hatujaona kumefanyika fairness. Tumeona watu wakisema hakuna ukabila kama wanavyosema Amerika, huku kwetu hatujaweza kuchukulia nationalism kama ilivyo kule. So kabla hatujafikia pale tuende kwa zile binu zetu za ki-Africa, na hatujafikia kile kiwango chao so wale ambao hawajajua took kabla gani nafikiri pengine wale experts wanaweza kusema hawa wataingia katika one side of unknown tribe. Asante.

Com Salome: Asante sana Muniri. Na sasa Tumefika mwisho wa kikomo cha siku yetu ya leo cha kikao hiki. Ningetaka kumuuliza mtu yoyote aliye na maadishi ama na maandiko hata kama hajazungumza, tafadhali apelike pale, utajisajiri na kuonyesha kuwa umetupatia maoni yako kwa maandishi. Ningetaka pia kuwajulisha pia Tume nzima ya mageuzi ya Katiba ya kuokoa wa Pwani kwa hivyo mumeona sisi tuko hapa, wengine wako kwenye vikao vya Bunge, vya mkoa huu na tuko kama siku saba hivi.

Mwisho ningetaka kuwashukuru nyote wakaaza wa kikao cha Mvita cha Bunge na ningetaka kuwajulisha kuwa tuko kwenye kikao hiki cha Bunge tena kesho, na kuwaalika tena, ikiwa kuna wale watapata nafasi ya kuja, waje tukutane kesho. Kina mama nimesikia mumesema mumejitayarisha kwa kikao cha kesho kwa hivyo ninaagalia, natarajia kukutana na nyinyi Quebaa Primary school.

Nataka tena kutoa shukrani kwa kufika mapema na kuweza kututafisiria, wenye wametusaikia na mitambo hii ya kupasia sauti ni kazi mingi na watu wengi, coordinator wetu wa hapa Mombassa wote wawili tunawashukuru sana na wafanyi kazi wetu wa kutoka Nairobi kwa matayarisho haya na washukuru na mwisho ninawashukuru wana Tume wenzangu.. Asanteni sana na Mungu awabariki.

Ningetaka kumuomba mtu mmoja atufungie kwa maombi. Kuna mtu anangetaka kutuomba. Uliinua mkono ungetaka kutuomba tafadhali.

Speaker: (Prayer Inaudible).

Meeting ended at 4.30 p.m.

&&&&&&&&&&&&&